# Nipashe

Ijumaa Februari 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580489

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Wazazi** mbaroni madai kumchoma moto mtoto wao

UKURASA 2



MAHOJIANO MAALUM -4

**Mwinyi:** Waliopewa ardhi kinyemela washughulikiwe

UKURASA 4



**Guardiola aisifia Man City kuweka rekodi**

UKURASA 20

MAGONJWA MLIPUKO

# Viongozi wawataka wananchi kujikinga

UKURASA 2

## Upandishaji mishahara kufanyika kimyakimya



UKURASA 3



Rais Dk. John Magufuli akizungumza na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Mkoa wa Morogoro, ili kujua changamoto zao, baada ya kulifungua, jana. **PICHA: IKULU**

# JPM aagiza waliokula fedha vizimba kurejesha

UKURASA 2







**MICHEZO** **SIMBA, AS VITA MECHI YA KISASI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Viongozi wawataka wananchi kujilinda

**Na Romana Mallya**

VIONGOZI mbalimbali wamesisitiza umuhimu wa Watanzania kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa ya milipuko na kutumia tiba asili kuyakabili.

Wakati wa uzinduzi wa Soko Kuu la Manispaa ya Morogoro jana, Rais John Magufuli alikumbusha umuhimu wa kuchukua hatua hizo, akibainisha kuwa hofu dhidi ya magonjwa ni hatari kuliko hata magonjwa yenyewe.

"Niwaombe wana Morogoro na Watanzania, tusimame imara, Mungu wetu yupo pamoja na sisi, tusiteteleke, tuchape kazi, tutumie mbinu hizi mbadala zinazojitokeza ikiwa ni pamoja na kujifukizia na kadhalika. Tutafaulu hili litapita, tuchape kazi, tusimame imara tuwe wamoja, tutapita na kuwa washindi," alisema.

Rais Magufuli alisema wakati wa tatizo la corona, nchi nyingi zilitangaza kujifungia, hivyo kwa vyovyote uzalishaji wa kiuchumi ulisimama katika nchi hizo.

"Ukishasimama, watu watapata shida ya njaa na chakula kwa sababu tumbo huwa halisamami kula, halijali wewe upo lockdown (umejifungia). Tuitumie hii nafasi Watanzania tulime mazao ya kutosha ya chakula na biashara.

"Ninawashukuru viongozi wa dini na Watanzania tumeendelea kumtanguliza Mungu katika magonjwa haya. Mungu ndiye jibu la kila kitu, Mungu ndiye mshindi wa kila kitu, tulifanikiwa mwanzoni, tutafanikiwa hata baadaye na siku zote tutafanikiwa kwa sababu Mungu yupo pamoja na Watanzania," alisema.

**KAULI YA MGANGA MKUU**

Katika tamko lake kuhusu kuimarisha mifumo ya udhibiti na kinga kwa magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza nchini juzi, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Abel Makubi, aidha, aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa bila kusubiri matamko ya viongozi wa serikali.

Vilevile, serikali itachukua hatua kali kwa hospitali zote za umma na binafsi zitakazopandisha gharama za matibabu katika kipindi hiki cha mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza nchini.

"Jambo hili si zuri kabisa kupandisha bei inakuwa kama vile msimu wa sikukuu za Krismasi ambapo mabasi yamekuwa yakipandisha nauli za abiria, nitoe onyo kwa yeyote atakayebainika, tutamchukulia hatua bila kujali ni kituo cha serikali au binafsi," alionya.

Prof. Makubi aliongeza: "Lazima wananchi mchukue tahadhari dhidi ya magonjwa haya ya kuambukiza na yasiyoambukiza bila kusubiri matamko, haiwezekani leo hii unaona kuna nyoka pale halafu bado unasubiri tamko."

Alisema katika kipindi cha Novemba hadi Aprili kila mwaka, huwa kuna ongezeko la magonjwa ya kuambukiza hususani yale yanayoambukiza kwa njia ya hewa na kuhara.

Alisema hali hiyo inatokana na mabadiliko ya hali ya hewa na mvua ambayo hunyesha katika msimu huo.

"Hivyo tunatakiwa kuchukua tahadhari zote muhimu za kujikinga na kujilinda na maambukizi kama ambavyo imekuwa ikishauriwa kila mara na wataalamu wetu wa afya," alisema.

Wakati viongozi hao wa serikali wakitoa rai hiyo, Mbunge wa Mbulu Mjini, Zacharia Isaay (CCM), ameitaka serikali kutoa tamko kuhusu kile alichodai kuwapo vifo vingi jimboni kwake.

Isaay alitaka majibu ya serikali jana bungeni jijini Dodoma, aliposimama kuchangia mjadala wa mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya mpango, bajeti ya serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2021/22 na mapendekezo ya mpango wa tatu wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano wa mwaka 2021/22 - 2025/26.

Mbunge huyo aliwataka wabunge kumuunga mkono kutokana na ukweli kuwa wanaoumia ni watu wao na kuna siku nao watarudi kuwa wananchi wa kawaida kama walivyo sasa wanaoumia.

"Mimi siwezi kuchangia kuhusu mpango, lakini ninaunga mkono kwa waliyochangia wenzangu. Mheshimiwa Spika, mimi ninataka kuzungumza juu ya vifo katika jimbo langu na ni ninaitaka serikali iseme kuliko kuficha, huu ugonjwa ni nini?"

"Serikali iache kigugumizi, jimboni kwangu watu wanakwisha Spika, nimechoka kuzika. Hata leo (jana) wanazika mtoto wa diwani, wakati mwingine ninashindwa kukuaga Spika kwenda Mbulu, ninaamua kutoroka," alisema.

Katibu Mkuu wa Kanisa la Anglikana (ACT), Mchungaji Dk. Mecka Ogunde, amewataka waumini wa kanisa hilo kuchukua tahadhari za kujilinda na magonjwa ya mlipuko katika nyumba zao za ibada.

Dk. Ogunde aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipofunga mafunzo ya vikoba kwa kinamama wa kanisa hilo kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Alisema kila mtu anaowajibu wa kuchukua tahadhari dhidi ya magonjwa hayo, ili kuendelea kubaki salama tofauti na ilivyo katika mataifa mengine.

Alisema tayari kanisa hilo limeshatoa miongozo pamoja na maelekezo mbalimbali katika makanisa yake juu ya kuchukua tahadhari kwa waumini wake.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akipata maelezo juu ya somo la sayansi kutoka kwa wanafunzi wa Taasisi ya Shule ya Msingi Kawe, alipotembelea maonyesho kwenye maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi Duniani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# JPM aagiza waliokula fedha kuzirejesha

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

RAIS John Magufuli, ameagiza watendaji wa Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa waliotwaa vizimba na maduka katika Soko Kuu jipya la Morogoro na kuwapangishia wafanyabiashara wadogo, warejeshe fedha mara moja.

Alitoa agizo hilo jana alipohutubia wananchi wa Manispaa ya Morogoro baada ya kulifungua rasmi soko hilo alilolipa jina la Chifu Kingalu, ili kutambua mchango wake kihistoria ikiwamo kuhamasisha uhifadhi wa mazingira na harakati za kupigania uhuru wa Tanganyika.

Rais Magufuli alisema baada ya kulifungua na kutembelea wafanyabiashara wadogo wa eneo lenye vizimba, alipata taarifa za kukodishiwa vizimba kwa gharama ya Sh. 50,000 na kulipishwa ushuru wa bidhaa ndani ya soko hilo.

Alisema kuwa akiwa ndani ya soko hilo, alipata ushahidi kutoka mfanyabiashara anayeitwa Said Ramadhani Alawi, kuwa amekodishiwa kizimba kimoja na mtumishi wa manispaa aliyemtaja kwa jina la Aika kwa Sh. 50,000 na kukilipia kwa muda wa miezi mitatu wakati mtumishi huyo anakilipia tozo halali ya Sh. 20,000 kwa mwezi kwa manispaa.

"Nimefungua soko ni zuri sana na nikapata nafasi ya kuwatembelea wafanyabiashara wa ndani ya soko, lakini nimeumia sana, nimeumia sana nilipofika kwenye vizimba baada ya kuelezwa na wafanyabiashara kuwa wamekodishiwa na watumishi wa manispaa kwa gharama ya Sh. 50,000 kwa mwezi.

"Meya upo hapa na umesikia hayo, hakikisha huyo Alawi anamilikishwa kizimba kuanzia leo na fedha zake alizochukua Aika, arudishiwe haraka na hilo pango sasa hivi alilipie manispaa na siyo kwa huyo mtumishi," aliagiza.

Rais Magufuli alitoa wiki moja kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya na uongozi wa manispaa pamoja na Meya na Mbunge wa Morogoro Mjini, kuhakikisha kero zote zilizoko kwenye soko zinamalizwa.

Vilevile, aliwakumbusha viongozi wa halmashauri zote na baraza la madiwani kuzingatia sheria zilizopitishwa na Bunge kutozivunja kwa kuanzisha sheria ndogo za halmashauri zinazokinzana na sheria mama ikiwamo tozo ya ushuru wa mazao.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo, alisema mradi wa ujenzi wa masoko 22 unafanywa kwa gharama ya Sh. bilioni 120 na mojawapo ya masoko hayo ni la Morogoro na kwamba tayari masoko tisa yamekamilika.

# Wazazi mbaroni madai kumchoma moto mtoto

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi mkoani Shinyanga linawashikilia Christina Mwangi na mume wake Yohana Michael, kwa tuhuma za kumchoma moto mtoto wao kwa madai ya kuiba karanga na kumsababishia majeraha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Debora Magiligimba, alisema tukio hilo lilitokea Februari 7, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana katika kijiji cha Usule wilayani Shinyanga.

Alisema jeshi hilo lilipata taarifa juu ya mtoto huyo kufanyiwa ukatili na wazazi wake kutoka kwa Mwenyekiti wa Mitongoji cha Usule, Peter Yohana.

Mwenyekiti huyo, alisema, aligundua mtoto huyo amefanyiwa ukatili huo kwa kuchomwa moto sehemu mbalimbali za mwili wake na baada ya kubaini, alifika eneo la tukio na kuwakamata watuhumiwa.

"Chanzo cha tukio la mtoto huyu kuchomwa moto na wazazi wake ni kudaiwa kuiba karanga ndipo wazazi wake Christina Mwangi ambaye ni mama yake mzazi na Michael, baba wa kambo, wakaamua kumpatia adhabu ya kumchoma moto sehemu mbalimbali za mwili na kumsababishia majereha makubwa," alisema Magiligimba.

Pia alisema mtoto huyo kwa sasa anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Shinyanga na hali yake ni mbaya kutokana na kuunguzwa moto.

# Mshahara kupandishwa kimya kimya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema haitatangaza hadharani upandishaji wa mishahara watumishi kwa kuwa itasababisha gharama za maisha kupanda na kuathiri makundi mengine.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Konde (ACT-Wazalendo), Khatibu Saidi Haji, katika kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Mbunge huyo alisema miongoni mwa ahadi zilizoko katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kupitia kauli za Rais ni juu ya uboreshaji wa maslahi ya wafanyakazi Tanzania.

"Wafanyakazi wa Tanzania wameendelea kuwa wavumilivu na wastahimilivu na wakijenga matumaini juu ya ahadi hii muhimu katika maisha yao. Je, serikali inatoa kauli gani ni lini wafanyakazi wa Tanzania watapandishiwa mishahara yao na kuboreshewa maslahi yao?" Alihoji.

Waziri Mkuu alisema serikali ya awamu ya tano ilipoingia madarakani ilijifunza kwamba wakati wote inapotangazwa hadharani kupandishwa kwa mishahara, kulikuwa kunatengeneza gharama kubwa kwenye masoko na kusababisha ugumu wa maisha kwa wananchi.

"Serikali inayo dhamira na inaendelea na dhamira hiyo ya kuboresha maslahi ya watumishi wa umma, tunalo eneo la mishahara, lakini upandishwaji wa madaraja na maeneo mengine pia." alisema.

"Tunao wafanyakazi lakini tunao wakulima, tunao wafugaji lakini tunao wavuvi. Hayo ni makundi mbalimbali lakini kwa eneo la wafanyakazi peke yake ukitangaza hadharani kwamba tumepandisha mishahara, kwenye masoko yetu, vituo vya mabasi na huduma zingine zote bei zote zinapanda," aliongeza.

Majaliwa alisema watu wanapandisha gharama hizo kwa sababu ya maslahi ya kundi moja tu, huku makundi mengine hakuna eneo la kupandisha maslahi yao.

"Kwa hiyo tumeona kwenye eneo hili tutumie njia ambayo si lazima tutangaze hadharani lakini tunaboresha maslahi ya wafanyakazi. Maslahi ya wafanyakazi hayako kwenye mishahara tu, tunapandisha madaraka na tunapunguza kiwango cha kodi, lakini pia kuna namna mbalimbali za kumfanya mtumishi kupandishiwa maslahi yake," alisema.

Hata hivyo, alikiri kuwa wafanyakazi wengi wanasubiri kusikia kupanda kwa mishahara, lakini kufanya hilo tayari unatengeneza ugumu wa maisha kwa sababu ya kupanda kwa vitu mbalimbali.

"Bado serikali inaendelea kutafuta njia nzuri ya kuongeza maslahi ya watumishi, Mheshimiwa Rais amesema mara kadhaa kupitia sherehe za wafanyakazi kwamba kupandisha mishahara kwa Sh. 20,000, Sh. 30,000 haina tija, lakini mara nyingi ukiamua kupunguza kodi ambayo mfanyakazi anakatwa kutoka kwenye tarakimu mbili kwenda kwenye tarakimu moja, lile ongezeko linaweza kuwa kubwa zaidi kuliko hili la kupandisha mshahara wa Sh. 10,000 na kuendelea," alisema.

Alifafanua kuwa bado Rais ameendelea kuwaahidi na serikali inaendelea kuwaahidi kuboresha maslahi ya watumishi wa umma kwa kuwa bado serikali ipo.

"Serikali imeingia madarakani tunatambua mchango mzuri sana unaotolewa na watumishi wa umma na serikali yao inatambua inapata mafanikio kwa sababu ya mchango wao mkubwa," alisema.

"Muhimu zaidi kupitia mabaraza ya wafanyakazi ambayo tunakaa nayo mara kwa mara na kujadiliana namna nzuri ya kuboresha maslahi, tunaendelea kukaa nao na zile taasisi na zile jumuiya za wafanyakazi kutafuta njia nzuri kuboresha maslahi ya wafanyakazi," alisema.

Aliwasisitiza wafanyakazi kuendelea kufanyakazi wakiamini serikali na wataendelea kuzungumza na mabaraza hayo juu ya kuboresha maslahi ya wafanyakazi.

## TMA yatoa tahadhari ya mvua, upepo mkali

**Na Faustine Feliciane**

WANANCHI wamepewa tahadhari kuhusiana na kuwapo mvua kubwa, upepo na mawimbi makubwa kwa baadhi ya mikoa kwa siku tano kuanzia jana.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana na Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) na kueleza kuwa mikoa itakayokumbwa na mvua kubwa ni Lindi, Mtwara, Ruvuma, Njombe, Mbeya, Iringa, Rukwa, Songwe na baadhi ya maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro.

TMA imesema kwa leo mikoa ya Dar es Salaam, Pwani (pamoja na visiwa vya Mafia), Tanga, Mtwara na Zanzibar itakumbwa na upepo mkali utakaofika mwendo wa kilometa 40 kwa saa pamoja na mawimbi makubwa yanayofika ukubwa wa mita mbili.

"Tunategemea kiasi cha kutokea kuwa cha wastani pamoja na madhara yake, hivyo wananchi wanapaswa kuchukua tahadhari na kwa wale wenye shughuli za uvuvi na usafirishaji majini pia kuchukua tahadhari na matukio yatakayotokea," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Aidha, TMA imesema itaendelea kufuatilia kwa karibu mabadiliko ya hali ya hewa na kutoa taarifa kwa wananchi.

Kadhalika, imevishauri vyombo vya habari vitumie taarifa rasmi inayotolewa na TMA kufikisha taarifa kwa wananchi ili kusaidia kuepuka maadhara yanayoweza kutokea.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akijibu maswali ya wabunge katika kipindi cha Maswali kwa Waziri Mkuu, Bungeni jijini Dodoma, jana. **PICHA: OWM**

## Wawekezaji kupigwa 'stop' uagizaji sukari

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Aldof Mkenda, amesema baada ya mwaka huu, serikali haitotoa vibali kwa wawekezaji waliopewa viwanda vya sukari kuagiza sukari nje.

Badala yake, Prof. Mkenda amesema kazi hiyo itafanywa na Bodi ya Sukari Tanzania. Prof. Mkenda alisema hayo jana katika kipindi cha Kumekucha kinachorushwa na ITV.

Alisema serikali imeanza kuchukua hatua za kudhibiti uagizaji wa sukari toka nje ya nchi kupitia kampuni ambazo ni wazalishaji kutokana na kuonyesha uzembe katika ununuaji miwa.

Waziri alisema upungufu wa sukari nchini unachangiwa na viwanda kushindwa kuongeza uwezo wa kuchakata miwa yote ya wakulima.

"Upungufu wa sukari nchini haukufanywa na upungufu wa miwa. Tatizo ni kampuni na wawekezaji kutokuongeza uwezo wa kuchakata miwa yote ya wakulima," alisema Prof. Mkenda.

Alisema takwimu za wakulima wa miwa katika Wilaya ya Kilombero kwa mwaka 2019/20 zilionyesha walizalisha wastani wa tani 900,000 za miwa wakati uwezo wa kiwanda cha sukari Kilombero ni kuchakata tani 600,000 hali iliyosababisha miwa takribani tani 300,000 kukosa soko na kuharibika.

Kuhusu ngano, Prof. Mkenda alisema tayari mkakati wa kuhakikisha zao hilo linalimwa kwa wingi umepatikana.

Alisema kwa sasa serikali iko katika mchakato wa kutia saini makubaliano na wafanyabiashara wakubwa wa ngano kununua asilimia 60 ya mahitaji yao ya ngano toka nchini.

"Tumekubaliana na wafanyabiashara wakubwa wa ngano kuwa kabla hawajaleta ngano toka nje, mfano ikiwa unaingiza asilimia 60, basi utalazimika kununua asilimia 60 ya ngano inayozalishwa ndani ya nchi kupitia taarifa itakayosaidia kukuza soko la wakulima wetu," alisema.

Prof. Mkenda alisema serikali iko katika utekelezaji wa mikakati ya kuongeza tija na kuhakikisha wakulima wananufaika na shughuli za kilimo ikiwamo uhakika wa masoko ya mazao.

Alisema kwa sasa bado kilimo kinachangia chini ya asilimia 30 kwenye pato la taifa wakati kinaajiri zaidi ya asilimia 70 ya nguvu kazi hali inayochangiwa na kuwapo tija ndogo kwenye kilimo.

"Tija bado ni ndogo sana katika kilimo hali inayosababisha wakulima walime eneo kubwa wakati mavuno wanayopata ni kidogo. Wizara tunajielekeza kukuza tija.

"Mfano sasa tunazalisha wastani wa tani 0.7 za ngano kwa hekta tofauti na wenzetu waliofikia tani 5.0 kwa hekta hali inayosababisha tuagize zaidi ya tani 800,000 za ngano toka nje," alisema.

HABARI KITAIFA

MAHOJIANO MAALUM -4

# Mwinyi: Waliopewa ardhi kinyemela washughulikiwe



Rais Hussein Ali Mwinyi. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Sanula Athanas,** ZANZIBAR

KATIKA sehemu ya tatu jana, Rais Hussein Ali Mwinyi alibainisha mikakati ya serikali yake kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia na udhalilishaji visiwani Zanzibar, ikijumuisha uanzishaji wa mahakama maalum ya kushughulikia kesi za ukatili na kufuta utaratibu wa dhamana kwa makosa ya aina hiyo.

Leo katika sehemu ya mwisho, Dk. Mwinyi, anazungumzia sekta ya ardhi, akiagiza mamlaka husika kuhakikisha watu wote waliopewa ardhi kinyemela, kuwalipa fidia wananchi walioondolewa katika maeneo hayo pasi na kupewa stahiki zao.

Pia anaagiza kurejeshwa serikalini kwa maeneo ambayo hayajaendelezwa na wawekezaji pamoja na yale ambayo baadhi ya viongozi walipeana kinyemela wakati wa kampeni za uchaguzi mkuu mwaka jana.

**SWALI: Yako malalamiko ya wananchi kupokwa maeneo yao na wawekezaji pasi na kulipwa fidia. Serikali yako imechukua hatua gani katika hili?**

**RAIS MWINYI:** Hili nimekutana nalo kwenye mikutano yangu na wananchi. Ni tatizo kubwa! Limesababishwa na kutofuata utaratibu. Utaratibu unataka pale mwekezaji mkubwa au mradi mkubwa wa serikali, lazima

**Tumeshazungumza nao, mwelekeo ni mzuri, wako tayari kutusaidia na mimi ninaamini kwamba tukienda na udhamini huo, tukahakikisha timu zetu zinapata udhamini, zitafanya vizuri zaidi.**

waliopo pale wafidiwe, tena wafidiwe vizuri!

Tuna lengo la kupiga vita umaskini, siyo kupiga vita maskini. Unapomwondoa mtu bila kumlipa fidia, unamwongezea umaskini.

Tunaendelea kuhakikisha kwamba wale wote waliopewa maeneo bila kufuata taratibu, bila kulipa fidia stahiki, basi wanafanya hivyo na wale ambao wamedhulumiwa tu kwa sababu mtu ana fedha au ana nguvu za madaraka, hao tutawarudishia ardhi yao.

Ni eneo ambalo ninalifanyia kazi na nimeagiza watendaji wote kuanzia kule chini kwa wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa, wahakikishe wanatenda haki kwa wale wananchi waliokuwa na maeneo yao hayo.

Pia si sahihi wananchi kukosesa ardhi huku watu wachache hasa viongozi wa serikali, wamehodhi maeneo makubwa.

Nimepewa taarifa kwamba wakati wa sisi tuko kwenye kampeni, kuna baadhi ya viongozi walikuwa wanagawana ardhi. Nimeagiza maeneo yote yaliyogawiwa, yarejeshwe serikalini na utaratibu uliotumika ufutwe. Siyo sahihi wananchi kukosa ardhi na kujigawia wao.

**SWALI: Serikali ya Umoja wa Kitaifa ndiyo maridhiano ambayo Wazanzibar walikuwa wanahitaji?**

**RAIS MWINYI:** Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeleta umoja, imeondoa kasoro zetu, sisi wanasiasa tumeweka pembeni kasoro zetu kwa mustakabali wa nchi yetu. Kwa hiyo, tunawataka na wananchi vilevile waache tofauti zao, waungane ili kuleta maendeleo.

Lakini Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni matakwa ya kikatiba. Katiba ya Zanzibar inasema kwamba chama kitakachopata kuanzia asilimia 10 ya kura nyuma ya chama kilichoongoza kwa kura katika Uchaguzi Mkuu, kitaingia kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Kwa kuwa Chama cha ACT-Wazalendo kilipata zaidi ya asilimia 10 ya kura, yalikuwa matakwa ya kikatiba. Kwa hiyo, tulikaa chini pamoja, tukakubaliana lazima twende hivyo ili kuilinda katiba yetu.

**SWALI: Ushirikiano ukoje katika Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa?**

**RAIS MWINYI:** Mzuri sana! Toka tumeanza, tunakwenda vizuri na ni mategemeo yangu kwamba tutaendelea kushirikiana vizuri. Makubaliano haya ni suala la kuwa na dhamira njema.

Mimi ninaamini sisi viongozi tuna dhamira njema, tuna nia ya kuunganisha watu ili kuleta maendeleo.

Sina shaka yoyote uhusiano huu utaendelea kwa sababu toka tumeanza, sijaona tatizo lolote na ni mategemeo yangu tutaendelea kwenda hivi mpaka tumalize kipindi chetu cha uongozi.

**SWALI: Timu za Zanzibar kwa sasa hazifanyi vizuri kwenye mashindano ya kimataifa. Serikali ya Awamu ya Nane inawapa matumaini yapi wananchi katika sekta hii?**

**RAIS MWINYI:** Niliwaahidi wananchi, na bahati nzuri safari hii tumefanya kampeni tukafika kwenye makundi yote. Wanamichezo nilikutana nao, wakanieleza changamoto zao na nikawaambia nitazifanyia kazi.

Moja ya vikwazo vikubwa ni ukosefu wa udhamini katika michezo, Unapokosa udhamini, maana yake ni kwamba hakutakuwa na fedha za kuendesha michezo. Kwa hiyo, niliwaahidi tutafanya mazungumzo na wawekezaji kutoka hapa Zanzibar na nje ya Zanzibar ili wadhamini ligi yetu ya soka na michezo mingine, siyo mpira wa miguu peke yake.

Tumeshazungumza nao, mwelekeo ni mzuri, wako tayari kutusaidia na mimi ninaamini kwamba tukienda na udhamini huo, tukahakikisha timu zetu zinapata udhamini, zitafanya vizuri zaidi.

Lakini hatutaishia kwenye udhamini tu. Serikali yangu imepanga kurudisha michezo kuanzia ngazi ya chini kabisa shule za msingi na sekondari, kujenga shule za michezo ili tuibue vipaji.

**SWALI: Katika kipindi cha uongozi wako, umepanga kuacha alama gani hasa?**

**RAIS MWINYI:** Kikubwa ni maendeleo. Wazanzibar wanachotaka ni hali nzuri ya maisha yao. Tunataka kuondoa umaskini wao. Na ili kulifanikisha hili, tunahitaji miundombinu ya kisasa, ajira zenye maslahi nzuri, huduma za jamii ambazo ni afya, elimu na maji ya uhakika.

Kwa hiyo, katika kipindi changu cha miaka mitano, kwa kadri Mungu atakavyoniwezesha, ninakusudia kupambana ili haya yote tunayoyazungumza yatimie.

Matumaini ni makubwa kwa sababu ndani ya kipindi hiki cha miezi mitatu, kampuni kubwa nyingi tu zimeonyesha nia ya kuja kuwekeza hapa Zanzibar.

Wito wangu kwa Wazanzibar tuendelee kudumisha umoja na amani tuliyonayo kwa sababu ndiyo msingi wa maendeleo. Tumelumbana kwa miaka mingi, hajatusaidia kitu. Sasa tuweke pembeni tofauti zetu na tuwe tayari kufanya kazi.

# TANGAZO


Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

## INVITATION TO TENDER

## TENDER No. TNRF/BMZ/ 1/02/2021

**1. Background**

The Tanzania Natural Resource Forum (TNRF) is a network organization registered in 2006 as a Non-Governmental Organization (NGO), with the aim of promoting the improvement of natural resource governance to achieve more sustainable rural livelihoods and better conservation outcomes. TNRF works for improved natural resources governance by helping bridge the gap between:

a) People's local natural resource management needs and practices, and
b) National natural resource management priorities, policies, laws and programs

TNRF has received funding from the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ) through World Wide Fund for Nature (WWF) Tanzania Country Office to implement some of activities within Climate change adaptation support for community managed areas (CBNRM) project aiming at supporting Protection of key ecosystems, increased resilience and adaptation for sustainable use by local communities. Enduimet, Makao, Lake Natron and Ikona WMAs have intact woodlands which are rich in blossom, bee keeping and has for many years been a traditional livelihood support activity. However, honey production to a commercial level has been hampered by the traditional approaches employed by communities including use of poor hives and destructive honey harvesting methods such as use of fires which sometimes cause wild fires and destroy the grasslands and vegetation for livestock and wildlife. This project thus will buy 800 beehives to be distributed in each WMA and will employ modern technology in bee keeping including procurement of 400 beehives and their accessories its supporting equipment i.e. (Honey harvesting kit, Solar wax extractor, Candle making machine and Honey extractor) to be used as bee hive fences to mitigate human-wildlife conflicts.

**TNRF thus invites bidders to supply the following:**

**Lot 1:** Supply of 200 beehives with its supporting equipment i.e. (Honey harvesting kit, solar wax extractor, Candle making machine and Honey extractor) to IKONA, and 200 beehives in MAKAO WMA

**Lot 2:** Supply of 200 beehives with its supporting equipment i.e. (Honey harvesting kit, solar wax extractor, Candle making machine and Honey extractor) to Enduimet WMA and
200 beehives Lake Natron.

Interested suppliers/firms may purchase tendering documents from TNRF offices, Plot # 10, Corridor Area, Arusha or via email: info@tnrf.org upon presentation of a request letter duly stating the company name and original bank slip/scanned for Tzs 100,000 (One Hundred Thousand Tanzanian shillings only) for each of the Lots mentioned above being a non- refundable fee. See our bank accounts details below:

Accounts Name: Tanzania Natural Resource Forum
Account No: 002 – 4002411.
*Bank Name: Absa Bank (T) Ltd, Arusha Branch*

All tenders in one original and one copy, properly filled and enclosed in plain sealed envelopes (Not indicating bidder's name) stating clearly TENDER FOR GOODS, SERVICE AND WORKS should be addressed to:

Procurement Tender Committee
Tanzania Natural Resource Forum
P.O BOX 15605,
Tel: +255747158888

ARUSHA-Tanzania

**TENDER No. TNRF/BMZ/01/02/2021**

Deposited at the reception of Tanzania Natural Resource Forum Offices, Plot # 10, Corridor

Area, Arusha.
Tender validity period is two weeks, ending 16th Feb, 2021 at 5.30pm

Jumuiko la Maliasili Tanzania
Tanzania Natural Resource Forum

## INVITATION TO TENDER

## TENDER No. TNRF/BMZ/ 2-6/02/2021

**CONSTRUCTION WMAs OFFICES, RANGER POST, RENOVATION OF TOURIST HOSTEL AND INFORMATION CENTRE**

**1. Background**

The Tanzania Natural Resource Forum (TNRF) is a network organization registered in 2006 as a Non-Governmental Organization (NGO), with the aim of promoting the improvement of natural resource governance to achieve more sustainable rural livelihoods and better conservation outcomes. TNRF works for improved natural resources governance by helping to bridge the gap between:

a) People's local natural resource management needs and practices, and
b) National natural resource management priorities, policies, laws and programs

TNRF has received funding from the Federal Ministry for Economic Cooperation and Development (BMZ) through World Wide Fund for Nature (WWF) Tanzania Country Office to implement some of activities within Climate change adaptation support for community managed areas (CBNRM) project aiming at supporting Protection of key ecosystems, increased resilience and adaptation for sustainable use by local communities. To strategically support operations of both Endumeit and MAKAO WMAs, improved infrastructure is very key to address the challenges they are facing like human wildlife conflicts, poaching and diminished income flow to sustain the operations of the WMAs in the light of COVID 19 and climate changes challenges.

**TNRF thus invite interested bidders for the following:**

**Lot 1**: Tender Code TNRF/BMZ/2/02/2021 Construction of office block for MAKAO WMA
at Mwangudo, Meatu district

**Lot 2:** Tender Code TNRF/BMZ/3/02/2021 Construction of two observation towers/ranger posts for MAKAO WMA; one at SAPA and second at Shugushi site, Meatu district

**Lot 3:** Tender Code TNRF/BMZ/4/02/2021 Construction of office block for Enduimet WMA
at Tingatinga, Longido District.

**Lot 4:** Tender Code TNRF/BMZ/5/02/2021 Construction of information center for
Enduimet WMA at Tingatinga, Longido District

**Lot 5:** Tender Code TNRF/BMZ/6/02/2021 Renovation of tourist hostel for Enduimet WMA
at Olmolog, Longido district

Interested suppliers/firms may purchase tendering documents from TNRF offices, Plot # 10, Corridor Area, Arusha or via email: info@tnrf.org upon presentation of a request letter duly stating the company name and original bank slip/scanned for Tzs 100,000 (One Hundred Thousand Tanzanian shillings only) for each of the Lots mentioned above being a non- refundable fee. See our bank accounts details below:

Accounts Name: Tanzania Natural Resource Forum
Account No: 002 – 4002411.
*Bank Name: Absa Bank (T) Ltd, Arusha Branch*

All tenders in one original and one copy, properly filled and enclosed in plain sealed envelopes (Not indicating bidder's name) stating clearly TENDER FOR GOODS, SERVICE AND WORKS should be addressed to:

Procurement Tender Committee
Tanzania Natural Resource Forum
P.O BOX 15605,
Tel: +255747158888

ARUSHA-Tanzania

**TENDER No. TNRF/BMZ/2/02/2021**

Deposited at the reception of Tanzania Natural Resource Forum Offices, Plot # 10, Corridor

Area, Arusha.

Deadline for application is 22nd February, 2021 at 05:30pm

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanafunzi 7,416 waliokacha shule serikali iwasake

**JUMLA** ya wanafunzi 7,416 waliochagulia kuingia kidato cha kwanza mwaka 2021 mkoani Shinyanga, hawajaripoti shuleni kutokana na sababu ambazo hazijaelezwa.

Kutokana na hali hiyo, Katibu Tawala wa Mkoa wa Shinyanga, Albert Msovela, amewataka wakurugenzi wa halmashauri, maofisa elimu na watendaji wengine wa serikali kuhakikisha ifikapo mwezi ujao wapeleke taarifa za wanafunzi hao.

Hali hii inajitokeza mwezi mitatu tangu kutangazwa kwa matokeo ya darasa la saba na wanafunzi kuanza masomo Januari, huku uhaba wa vyumba vya madarasa na madawati ukiwa ni tatizo kubwa.

Hadi sasa haijulikani wanafunzi hao wako wapi, lakini kutokana na matukio ya ndoa za utotoni na utumikishwaji wa watoto mkoani humo, huenda baadhi wameshaozeshwa au kwenda kufanya kazi.

Takwimu hizi zinaonyesha bado kuna kazi kubwa ya kufanya kwa viongozi wa mkoa huo kwa kushirikiana na asasi zisizo za kiraia, katika kuhakikisha wanafunzi hawa wanajulikana waliko na wanafanya nini ili warudishwe shuleni kuanza masomo.

Wadau muhimu ni wazazi ambao moja kwa moja wanajua waliko watoto wao na walikuwa na nafasi kubwa ya kuhakikisha wanahudhuria masomo na siyo kwenda walikokwenda.

Sheria inakataza kumwozesha mwanafunzi au kumkatisha masomo kwa sababu nyinginezo na hatua kali za kisheria zimetajwa ikiwamo jela miaka 30, ni muhimu sheria ikachukua mkondo wake ili kuhakikisha watoto wanapata haki.

Pia, ni muhimu mkoa kuongeza jitihada za kupambana na matukio ya ukatili kama ndoa za utotoni ambazo mkoani humo zimeongezeka na kutajwa katika takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA).

Tunaamini mamlaka zote za serikali zikishirikiana na Asasi za kiraia pamoja na wazazi watajua waliko wanafunzi hawa na kama kuna umuhimu wa kuchukua hatua ni vyema kufanya hivyo.

Pia, takwimu hizi zinaonyesha kuwa bado kuna kazi kubwa ya kufanya ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto.

Kwa sasa hakuna sababu za kuwapo kwa ada au michango kwa kuwa elimu ni bure, kinachotakiwa ni mzazi kuhakikisha anapata mahitaji muhimu kama sare za shule, viatu, madaftari na kalamu.

Ikumbukwe kwamba hivi sasa serikali inatoa kiasi cha shilingi bilioni 23 kila mwezi kwa ajili ya kugharamia elimu bure kwa wanafunzi wa elimu ya msingi hadi sekondari kidato cha nne.

Katika kukabiliana na tatizo hili, tunaona kwamba ni wakati mwafaka sharia zilizopo kutumika kuwabana wote watakaobainika kwa njia moja ama nyingine kuwa kikwazo kwa elimu ya watoto wetu.

Ni muhimu wazazi wasikimbie wajibu wao wa msingi katika kuhudumia watoto, na watambue kuwa elimu ni lazima na siyo hiari kwa kuwa mbali na mtoto kuwa wake, lakini ni mali ya serikali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Tanzania ya Viwanda iwe fursa vijana kujiwekeza kwenye kilimo

**HAPA** nchini kumekuwapo na wimbi la baadhi ya vijana kukimbilia mijini, huku wakiamini dhana kwamba ndiko kwenye maisha rahisi na kupatikana fedha ni mwepesi kuliko vijijini wanaokotoka.

Katika mazingira hayo, vijana hao wanajikuta wanaambulia kufanya biashara ndogo, zikiwamo za pipi, biskuti, karanga na zinazofanana nazo, hasa pale wanaponashindwa kumudu pilika za maisha.

Wakifanya hivyo, huku wakiacha kilimo kikiwa ni uti wa mgongo wa taifa, kwa kuwa kinatajwa kuajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania. Hapo kuna mchango mkubwa katika pato la taifa.

Kukimbilia kwao mijini kunaonyesha vijana hawajaona fursa zilizopo kwenye kilimo, au kutothamini kilimo kutokana na changamoto zake, hasa pale wanaotegemea msimu wa mvua.

Pamoja na changamoto hizo, ni vyema vijana wakatambua kuwa wakati huu ambao Tanzania inaeingia kwa na Uchumi wa Viwanda, ipo haja sasa kada hiyo ya umma ikabadili mawazo na kuamua kujikita vijijini, kuendeleza kilimo badala ya kuendelea kukimbilia mijini na kujikuta wakikwama.

Ni kweli, bado kuna changamoto nyingi kwenye kilimo na hasa kile cha kutegemea msimu wa mvua, lakini bado wanaweza kupata manufaa kuliko biashara wanazofanya mijini.

Kimsingi ni kwamba, vijana hawatakiwi kukata tamaa, waendelee kujiajiri katika fursa walizo nazo zikiwamo ardhi ya kilimo kwa kutumia nguvu walizobarikiwa na Mungu, kwa vile serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kilimo.

Ikumbukwe kuwa, serikali imeamua kuwainua wakulima ikiwa ni pamoja na kutaifisha mashamba makubwa yaliyokuwa hayatumiki na kuwagawia wakulima, hivyo ni fursa kwa vijana kuchangamkia fursa hiyo.

Inaelezwa kuwa, Tanzania ina eneo kubwa linalofaa kwa kilimo, lakini bado linalotumika ni dogo, kutokana na kwamba watu wengi hasa vijana, hawajatambua fursa hiyo na badala yake wanajikuta katika umachinga tu.

Hiyo ni kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (CEGODETA), Thomas Ngawaiya, kwamba kukimbilia mijini kufanya biashara ndogo kumepitwa na wakati.

Ni kweli kwamba mtindo huo umepitwa na wakati, kwa kuwa katika kilimo ndiko kwenye malighafi za viwandani, hasa ikizingatiwa kuwa nchi inaelekea kuwa viwanda na wazalishaji mali ni vijana wenyewe.

Binafsi ninaamini kwamba, vijana wenye nguvu ya kufanya kazi hawawezi kushindwa kulima mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara, hivyo cha msingi ni wao kubadili mwelekeo na kuachana biashara ndogo.

Hivyo vijana wanaotoka kwenye mikoa inayozalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula na biashara, ni vyema wakafakari na kuangalia uwezekano wa kuacha mawazo ya kukimbilia mijini.

Kwa mfano, korosho ni miongoni mwa mazao ambayo huliwa na watu wengi na mara nyingi hata kwenye vikao vya watu wazito, ni rahisi kuzikuta zimewekwa mezani au zikitafunwa.

Hivyo, kwa vijana wanaotokea mikoa inayolima zao hilo, ni vyema wakatumia nguvu zao kujikita kwenye kilimo cha korosho, kwa kuwa linahitajika na linaweza kuwaingizia kipato.

Lakini kikubwa zaidi ni kwamba, malighafi za Tanzania ya viwanda zinatokana mashambani na watu wengi nguvu za kuzalisha mali ni vijana, hivyo wasiache fursa hiyo na kukimbilia mijini kufanya biashara ambazo hazina maslahi.

Mtindo wao wa kukimbilia mijini unasababisha umaskini katika familia, kutokana na ukweli kwamba wanaacha wazazi wasio na uwezo wa kulima, hivyo kujikuta hawana chakula na huduma nyingine za msingi.

Nguvu zao ambazo zingetumika kuzalisha mali mashambani, zinakuwa ni za kuzurura mitaani kwa biashara ndogondogo huku wazazi na walezi wakikosa msaada wao wa kulima na kuzalisha mazaao ya chakula na biashara.

# ZIARA YA MKURUGENZI MTENDAJI WA TPDC VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Meneja wa kiwanda cha uchapishaji cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Balasubramaniyan Venkadachalam, akifafanua jambo kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika hilo, Dk. James Mataragio (wa pili kushoto), alipotembelea kiwandani hapo. Wa tatu kulia ni Mkurugenzi wa IPP, Joyce Luhanga. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul (kushoto), akitoa maelezo kwa Dk. James Mataragio, jinsi taarifa ya habari inavyorushwa ndani ya studio ya televisheni hiyo.



Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Mauggo (kulia), akimkaribisha Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dk. James Mataragio (kushoto), na Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa shirika hilo, George Seni, walipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana.



Mwandaaji wa vipindi na mtangazaji wa East Africa Radio, Irene Tillya (kulia), akifafanua jambo kwa wageni hao, walipotembelea studio za redio hiyo.



Dk. Mataragio (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi wa Capital Radio, Abdalla Mwaipaya (kulia), ndani ya studio ya redio hiyo. Wa (tatu kulia) ni Mkurugenzi wa Fedha na Utawala wa shirika hilo, George Seni.



Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/Radio One, Joyce Mhavile (wa pili kushoto), akifafanua jambo kwa wageni hao.

## HABARI KITAIFA

# OUT yazidi kumbana makamu mkuu wake

**Na Elizabeth Zaya**

BARAZA la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), kimemtaka Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Elifas Bisanda, kuiomba radhi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na mamlaka husika kwa kutoa taarifa ya tahadhari ya ugonjwa wa corona pasipo kufuata taratibu na mwongozo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Rasilimali Watu), Prof. George Oreku, baraza hilo nalo limeomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza kutokana na taarifa iliyotolewa na Makamu Mkuu huyo.

"Katika kikao chake cha dharura kilichofanyika Februari 10, mwaka huu, Baraza la Chuo Kikuu Huria cha Tanzania lilipokea na kujadili waraka wa Makamu Mkuu wa Chuo juu ya tahadhari ya maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 uliotolewa Februari 8, mwaka huu, kwa wafanyakazi na wanafunzi wa chuo," alisema Prof. Oreku.

"Baraza lilibaini kuwa sehemu kubwa ya waraka huo ni maoni binafsi ya Makamu Mkuu wa Chuo pia alikosea kutumia nembo ya serikali," alisema.

Pia Prof. Oreku alisema baraza limejiridhisha kuwa Prof. Bisanda alikosea kuandika taarifa bila takwimu na kuthibitisha uhalali wa baadhi ya taarifa hizo alizozitoa.

"Baraza lilijiridhisha kuwa Prof. Bisanda alikosea kuandika taarifa husika bila takwimu na kuthibitisha uhalali wa baadhi ya taarifa hizo na lilibaini kuwa inakinzana na miongozo na sera ya serikali juu ya tahadhari ya ugonjwa COVID -19 kwa serikali na taasisi za elimu.

"Pia inakinzana na mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa huo katika shule, vyuo na taasisi za elimu nchini wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto wa Mei 27, 2020," alisema.

"Hivyo basi baraza limetoa maagizo kwa Makamu Mkuu wa Chuo, aombe radhi kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, mamlaka husika na umma. Baraza pia linaomba radhi kwa usumbufu uliojitokeza."

"Wafanyakazi na wanafunzi wa OUT waendelee na kazi na masomo kama kawaida," alisema Prof. Oreku katika taarifa hiyo.

Baraza hilo liliwakumbusha wafanyakazi na wanafunzi wa chuo hicho kuhusu miongozo ya kupambana na maambukizi ya virusi vya COVID-19 kama ilivyotolewa na serikali.

Taarifa hiyo ya Baraza la OUT ya kumtaka Prof. Bisanda kuomba radhi, inakuja ikiwa tayari Wizaya ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiwa imeshatoa tamko la kumkana makamu huyo ya chuo na kuwataka wanafunzi na wafanyakazi kuendelea na kazi na masomo kama kawaida.

Juzi, Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Wizara hiyo, Oliva Kato, alisema waraka uliotolewa na Prof. Bisanda ni batili na maelekezo aliyoyatoa ni maoni yake binafsi na kwamba hayakuzingatia mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya ugonjwa wa corona.



Mratibu wa Miradi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Hellen Urio (kushoto), akizungumza na wanafunzi katika maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Ukeketaji, yaliyofanyika eneo la Kivule, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Balozi kufundisha wageni Kiswahili

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameagiza balozi zote za Tanzania zilizopo nje ya nchi, kuanzisha kituo cha wageni kujifunza Kiswahili.

Kwa sasa, malengo ya serikali ni kupanua matumizi ya lugha ya Kiswahili, baada ya kukiingiza katika diplomasia.

Akijibu swali aliloulizwa na Mbunge wa Kawe (CCM), Askofu Josephat Gwajima, katika kipindi cha maswali ya papo kwa papo Bungeni jijini Dodoma jana, Majaliwa alisema lugha ya Kiswahili imeenda mbali zaidi na kutumiwa na nchi za Ujerumani, Marekani, lakini hata pia Uingereza na mataifa mengine makubwa.

"Sisi kama serikali tumewasiliana kupitia balozi zetu. Kila Balozi tumeagiza kuanzisha kituo cha ku-engage (kuhusisha) wageni wenyeji mahali ambapo Balozi yupo kuanzisha kituo cha kujifunza Kiswahili.

"Malengo yetu ni kupanua matumizi ya lugha ya Kiswahili, tunapoagiza mabalozi kufungua kituo ni kuwafanya nchi husika kufundisha Kiswahili ambacho sasa tumekiingiza katika diplomasia.

"Na kwa kuwa Kiswahili kinapendwa duniani kote, sasa sisi Watanzania tuna fursa ya kuwa walimu wazuri kwenye nchi hizo na kwenye vituo vyetu vile vya kufundisha Kiswahili."

Kabla ya majibu hayo ya Waziri Mkuu, Askofu Gwajima, alisema lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha 10 zinazozungumzwa sana Barani Afrika, ni lugha ya pili kwa kuzungumzwa na watu wengi barani Afrika na ni kati ya lugha 10 zinazozungumzwa sana duniani. Je, serikali ina mkakati gani kuhakikisha Kiswahili kinakuwa bidhaa hasa katika kuchangia diplomasia ya uchumi na kuwa fursa ya ajira kwa Watanzania?

Katika majibu yake, Waziri Mkuu, alisema wanapopelekwa walimu kwenye nchi hizo tunafungua fursa kiuchumi kwa kuajiri watu na Watanzania kwenda kufanya kazi kwenye nchi hizo.

Alisema baada ya kufunguka kwa fursa za ajira, kodi kidogo itarudi nchini na kuboresha uchumi wa ndani.

Vile vile, alisema serikali itatumia diplomasia hiyo kujenga uchumi wa ndani na kuvuta Watanzania kuajiriwa katika maeneo hayo ili kuboresha Kiswahili.

## Kampeni saratani yaongezewa nguvu

**Na Christina Mwakangale**

TAASISI ya Aga Khan, kupitia Mradi Mtambuka wa Saratani Tanzania (TCCP), imekabidhi mashine ya kisasa ya radiolojia (ultra sound) kwa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), itakayosaidia kugundua mapema ugonjwa wa saratani.

Mashine hiyo yenye thamani ya Sh. mil. 115, ni sehemu ya mradi wa TCCP ambao unatekelezwa nchini kwa miaka minne utawafikia Watanzania milioni 1.7 kwenye vituo vya huduma za afya 100, mkoani Mwanza na Dar es Salaam.

Mkurugenzi Mtendaji wa ORCI, Dk. Julius Mwaiselage, akizungumza jijini jana, baada ya kupokea msaada huo, alisema mashine hiyo itaongeza kasi ya uchunguzi kwa wagonjwa kutoka 50 hadi 80 kwa siku.

Alisema kupitia TCCP, huduma za hospitali hiyo zitaboreshwa na kwamba kwa mwaka, wagonjwa 43,200 hufanyiwa tiba ya mionzi.

"Mradi huu utaongeza kiwango cha huduma ikiwamo afya, kutoa elimu na kufanya utafiti. Wagonjwa wote ni lazima kutumia 'ultrasound' kujua ugonjwa hali ya maendeleo yake, hadi sasa tuna mashine za kisasa tatu," alisema na kuongeza:

"Mashine hii ni maalum kuangalia uvimbe ni aina gani, wa saratani au la. Pia muda wa kusubiri majibu itakuwa saa 12 hadi 24 kutoka saa 48, kama ilivyokuwa awali."

Meneja Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Omary Ubuguyu, alisema kuboreshwa huduma za kibingwa nchini, kumeokoa maisha ya Watanzania.

"Ukiangalia hali ilivyo sasa duniani safari za nje nchi tofauti zimesimama, tulitegemea tiba nje kama vile India, tusingekuwa na ubora ilivyo sasa tungepoteza wengi, tumehudumia sasa," alisema Dk. Ubuguyu.

## Benki ya Stanbic yaunga mkono Siku ya Wanawake

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic Tanzania imechangia shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuunga mkono maadhimisho ya siku ya kimataifa ya wanawake na mabinti kwenye sayansi katika hafla iliyoratibiwa na shirika la Vijana Think Tank.

Mchango huo umelenga kutambua shughuli kubwa inayofanywa na wanawake na mabinti kwenye sayansi na teknolojia, pamoja na kuhimiza jinsia ya kike kuzidi kushiriki na kuzipenda kozi za sayansi, teknolojia, uhandisi na hesabu (STEM), ambazo zina mchango kubwa katika kufikia ajenda ya maendeleo ya viwanda pamoja na kupunguza mwanya uliopo wa kijinsia.

Tanzania pamoja na mataifa mengine yanayoendelea yanatambua kuwa sayansi, teknolojia na uvumbuzi ni maeneo yenye mchango mkubwa katika kuleta maendeleo ulimwenguni pamoja na maendeleo ya Viwanda. Benki ya Stanbic Tanzania kupitia ushiriki wake imeweza kubaini kuwa bado kuna idadi ndogo ya mabinti ambao wameandikishwa kwenye kozi za STEM katika vyuo mbalimbali.

Kwa mujibu wa data za Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na Elimu, Sayansi na Tamaduni (UNESCO), asilimia 24 kati ya 40 ya wanawake ndio wamebainika kujiandikisha kwenye kozi za sayansi, uhandisi na teknolojia vyuoni. Mwanya ambao umeendelea kuwazibia nafasi wanawake kuweza kunufaika na fursa za ajira zilizopo sasa na baadae, wakati dunia ikiendelea kujikita kwenye mifumo kamili ya kidigitali na uvumbuzi wa teknolojia.

Akizungumzia mchango wa Benki ya Stanbic, Mkuu wa Huduma za Benki Binafsi na Kibiashara, Omari Mtiga, alisema kuwa, "Ili taifa liendelee na liweze kufikia ajenda ya viwanda, ni lazima idadi ya wanawake wanaoandikishwa kwenye masomo ya sayansi, teknolojia na uvumbuzi iongezeke. Hii ni pamoja na kuboresha mbinu za kuwavuta wanawake kujiandikisha kwenye taaluma hizi. Ushirikiano huu ni moja ya kampeni za kijamii ambazo benki inaendelea kushiriki ili kuwahakikishia vijana kuwa, kupitia bidii, malengo na kujiendeleza wanaweza kufikia ndoto zao."

Mtiga aliongeza kuwa, ukuaji wa kiuchumi unategemea sana matumizi mazuri ya mtaji wa watu waliopo. "Ili Kufanikiwa kuwa na usawa wa kijinsia katika eneo hili, sekta zote zinapaswa kuunda ushirikiano wenye kuwapa nguvu wanawake, mabinti na vijana wote ili kuwahamasisha waweze kushiriki na kuipenda sayansi."

# AAR yaanzisha mfumo wa kuboresha huduma za bima

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya AAR Insurance Tanzania imezindua rasmi mfumo wa 'smart health', unaolenga kuboresha huduma kwa wateja na utendaji katika sekta hiyo.

Uzinduzi huo ulifanyika jana , jijini Dar es Salaam. Tukio hilo lililohudhuriwa na mawakala wa bima, na wadau wengine wa afy,a lilitumika kutoa elimu zaidi kuhusu ufanisi na faida za mfumo huo ulioanzishwa mwaka 2020.

Akizungumza na vyombo vya habari wakati wa tukio hilo, Afisa Mkuu wa Operesheni (COO) wa AAR Insurance, Dk. Emmanuel Bwana, alisema kuwa kampuni hiyo imetumia maendeleo ya teknlojia kuhakikisha kuwa wateja wao wanapata huduma bora zaidi ya bima ya afya, kwa wakati na kwa urahisi.

**Hatua hii ni sehemu ya mchango wetu usiokoma kuunga mkono jitihada za serikali na wadau wengine katika kuhakikisha kila mmoja katika jamii anapata huduma bora ya bima ya afya.**

"Hatua hii ni sehemu ya mchango wetu usiokoma kuunga mkono jitihada za serikali na wadau wengine katika kuhakikisha kila mmoja katika jamii anapata huduma bora ya bima ya afya," alisema.

"Mfumo huu wa 'smart health' utawasaidia mawakala kutoa huduma kwa wakati na katika mazingira waliyopo wakiwa na mteja papo kwa papo. Kwahiyo, hakutakuwa na ulazima kwa wakala wa bima ya afya kupiga simu AAR ili aweze kupewa taarifa (quote)," aliongeza.

Kwa mujibu wa Dk. Bwana, kwa msaada wa mfumo huo, mteja anaweza kuingia kwenye mfumo na kupata taarifa mbalimbali ambazo ni pamoja na historia au kumbukumbu za madai yake na faida nyingine zilizopo wakati huo.

Mmoja kati ya washiriki wa mafunzo hayo, ambaye ni wakala wa bima ya afya ya AAR, Peter Sekdia, aliipongeza kampuni hiyo akieleza kuwa mfumo huo utawasaidia kuongeza ufanisi katika kutoa huduma kwa wateja. Alifafanua kuwa mfumo utaongeza kasi ya kupokea taarifa kutoka kwa mteja, itaowaongezea watoa huduma kasi ya kuthibitisha uhalali wa mteja na kadhalika.

"Tukio hili limenifanya niione siku bora zaidi katika sekta hii ya afya, kila kitu kimerahisishwa na kila mdau wa afya atafaidika na mfumo. Tunaipongeza AAR Insurance kwa kuanzisha mfumo huu. Kwakweli, utaboresha maisha ya watu wengi nchini na hata nje ya mipaka ya nchi yetu," alisema.

Hatua ya Kampuni ya AAR Insurance kuanzisha mfumo wa smart health unaakisi jitihada za dunia katika kufanikisha mfumo wa bima ya afya unaotolewa moja kwa moja kwa njia ya mtandao (eHealth System).



Washiriki wa mafunzo ya mfumo wa 'smart health', yanayotolewa na Shirika la Bima la AAR, unaolenga kuboresha huduma kwa wateja na utendaji katika sekta hiyo wakipata mafunzo hayo jijini Dar es Salaam jana. **MPIGAPICHA WETU**

## Ufuta wawapa wakulima bil. 25/-

**Nas Mwandishi Wetu**

WAKULIMA wa ufuta mkoani Ruvuma wamelipwa zaidi ya Sh.bilioni 25 baada ya kuuza kilo 12,234,757 ya zao hilo kupitia mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani kuanzia msimu wa mwaka 2018/2019 hadi 2019/2020.

Mkuu wa Mkoa huo, Christina Mndeme, alisema katika kipindi hicho wakulima pia waliuza kilo 4,260,777 zilizowaingizia zaidi ya Sh. bilioni 2.585.

"Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa ambayo imekuwa inatekeleza mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, pia tuna mazao mawili ya kimkakati ambayo ni korosho na kahawa, yamekuwa yakiuzwa kupitia mfumo huu,"alisema Mndeme.

Amesema mfumo huo umewanufaisha wakulima kwa kupata soko la uhakika na bei nzuri ya mazao yao, na kwamba shughuli za kilimo katika msimu wa mwaka 2020/2021 zinaendelea vizuri ambapo wakulima wamelima mazao mbalimbali.

Kuhusu mbolea, alisema Mkoa kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mbolea Tanzania (TFRA), unaendelea kusimamia upatikanaji wa mbolea ili wananchi waweze kuzalisha chakula cha kutosha.

## Umwonapo toa taarifa

**Na Christina Mwakangale**

MARIAMU Juma (22), ambaye ana tatizo la afya ya akili anatafutwa na wazazi wake baada ya kutoweka nyumbani kwao kwa zaidi ya miezi minne iliyopita.

Baba yake mlezi, Ayubu Rubale, akizungumza na Nipashe jana, jijini Dar es Salaam, alisema, Mariamu alitoweka nyumbani Septemba 8, mwaka jana.

"Tunaishi mtaa wa Kipilipili, Salalasa, Wilaya ya Kinondoni, alikuwa kama karukwa na akili na kuruka ukuta, pamoja na kufuatilia maeneo yote ya jirani hatujampata ni zaidi ya miezi mitatu sasa," alisema Rubale.

Alisema taarifa ya kupotea kwake ilitolewa katika Kituo cha Polisi Salasala na kupatiwa namba **RB/SLS/663/2020**. Aliongeza kwamba atakayemwona, atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo jirani naye na kupiga simu namba **0713 730954** na **0767 230056**.

# Serikali yawaruka wanaotoza wajawazito




Habari na Augusta Njoji

BUNGE limeelezwa kuwa serikali haijatoa maelekezo kwa watendaji na watoa huduma za afya kutoza faini kwa wajawazito wanaojifungulia nyumbani.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dk. Festo Ndugange aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA), Grace Tendega. Mbunge huyo alitaka kujua kauli ya serikali kuhusu wajawazito wanaojifungulia njiani au nyumbani kutozwa faini ya Sh. 50,000 hadi 70,000.

Tendega alisema imekuwa ahadi ya muda mrefu ya kujenga sehemu za wajawazito kusubiria na kwamba kwenye sera ya afya serikali inasema itajenga vituo vya afya kila kata na zahanati kila kijiji.

"Katika jimbo la Kalenga hii ni kero kubwa na kinamama wakijifungulia njiani au nyumbani wanatozwa faini ya Sh. 50,000 hadi 70,000. Ni lini serikali itajenga majengo haya na nini kauli ya serikali kuhusu faini hizo wanazotozwa wajawazito?" alihoji.

**Imekuwa ahadi ya muda mrefu ya kujenga sehemu za wajawazito kusubiria na kwamba kwenye sera ya afya serikali inasema itajenga vituo vya afya kila kata na zahanati kila kijiji.**

Dk. Ndugange alisema serikali haijatoa maelekezo hayo na kwamba ni wajibu wa watendaji katika mamlaka za serikali za mitaa kutoa elimu na kuhamasisha wajawazito kuona umuhimu wa kujifungulia katika vituo vya kutoa huduma badala ya kuwalipisha faini ya kujifungulia nje ya vituo.

Naibu Waziri huyo alisisitiza wajawazito kuendelea kujifungulia kwenye vituo vya kutoa huduma za afya.

"Ni kweli tunahitaji kupunguza vifo vya kinamama na watoto kwa kuboresha miundombinu ya afya, miradi ya ujenzi wa majengo ya kujisubiria ni kipaumbele cha serikali na yanajengwa ili kupunguza umbali wajawazito kufika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya," alisema.

Ili kujenga majengo hayo, alisema lazima kuwe na kituo cha afya ndiyo sababu serikali inajenga kwa wingi vituo vya afya karibu na makazi ya wananchi na yale maeneo yenye umbali mkubwa kuweka mpango wa pili wa kujenga majengo ya kujisubiria wajawazito.

"Haitakuwa na tija sana kujenga majengo ya kujisubiria bila kuwasaidia wananchi wanaokabiliwa na umbali mkubwa kufuata huduma za afya. Kipaumbele namba moja lazima uwe na kituo. Katika miaka hii mitano ndio maana serikali imejenga vituo vingi na tunaendelea na ujenzi huo kusogeza huduma kwa wananchi na baadaye tutajenga majengo ya kujisubiria," alisema.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji mkakati wa serikali wa kujenga maeneo ya kusubiria kujifungua katika vituo vya afya. Naibu Waziri huyo alisema serikali imeendelea kutekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya nchini, utekelezaji wa mpango huo umesaidia kuboresha upatikanaji wa huduma za afya ya msingi na kusogeza huduma za afya karibu na wananchi kwa lengo la kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga katika maeneo ya vijijini.

"Kuanzia mwaka 2015 hadi Septemba, mwaka jana, serikali imejenga zahanati 1,198, imejenga na kukarabati vituo vya afya 487 na hospitali 102 za halmashauri zimejengwa," alisema.

Alisema mpango wa ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya umesaidia kuongeza idadi ya kinamama wanaojifungua kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kutoka kinamama 1,383,342 mwaka 2015 hadi 1,896,136 mwaka 2020.

Hata hivyo, alisema serikali katika bajeti ya mwaka wa fedha 2020/21 imeendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuongeza vituo vya kutolea huduma za Afya ambapo, zimetengwa Sh. bilioni 27.75 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya zahanati 555 ili kusogeza huduma karibu na wananchi.



Mbunge Mteule kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Amer Abdallah Amer, akila kiapo cha uaminifu cha Ubunge mbele ya Spika wa Bunge, Job Ndugai, Bungeni jijini Dodoma jana. Kulia ni Katibu wa Bunge, Stephen Kagaigai. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Wahandisi wazawa washiriki miradi mikubwa

SERIKALI imesema kuna wahandisi wahitimu 197 ambao wanashiriki katika miradi mikubwa ukiwamo wa kufua umeme katika Bwawa la Mwalimu Nyerere na mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR).

Aidha, imesisitiza kuendelea kuweka mfumo wa kuhakikisha katika miradi mikubwa inayotekelezwa nchini, suala la kubadilishana weledi linaendelea kupewa kipaumbele.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mhandisi Mwanaisha Ulenge.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema miradi mikubwa ya ujenzi nchini inafanywa na kampuni kutoka Asia wakati wahandisi nchini wanasoma kwa mitaala ya Uingereza na Marekani.

"Je, Serikali haioni haja ya kuongeza mitaala ya Asia katika mitaala ya Vyuo vya Uhandisi ili wahandisi wetu wapate utaalam katika miradi ya ujenzi?" alihoji.

Pia alihoji suala la kubadilishana uweledi limepewa kipaumbele gani katika miradi inayoendelea kujengwa hapa nchini.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Kipanga alisema uhandisi ni fani ya kimataifa ambayo mitaala yake haitofautiani kijiografia.

"Kwa muktadha huo, mitaala ya shahada za uhandisi katika vyuo vyetu nchini nayo ni ya viwango vya kimataifa. Hata hivyo, ni kawaida kuhuisha mitaala mara kwa mara ili kuingiza utaalamu mpya kwenye fani," alisema.

Alibainisha kuwa nia ya serikali kuhuisha mitaala ya kihandisi na fani nyingine za kipaumbele kwenye Tanzania ya viwanda kama tunavyoongozwa na Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) 2020-2025 inaagiza "kuhuisha mitaala na kuanzisha programu kulingana na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa ili wahitimu wawe na stadi stahiki za kumudu kufanya kazi mbalimbali za kuajiriwa na kujiajiri na hasa kwa kuzingatia mapinduzi ya nne ya viwanda.

Hata hivyo, alisema suala la kubadilishana weledi wa kihandisi katika miradi mikubwa inayoendelea tayari linatekelezwa ambapo wahitimu wa uhandisi hupata nafasi za utarajali katika miradi mikubwa ya kitaifa ili kupata uweledi.

# Utafiti wabaini viashiria madini

WIZARA ya Madini kupitia Wakala wa Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kwa nyakati tofauti imefanya utafiti wa awali katika maeneo mbalimbali zikiwamo kata za Makuru, Solya, Kintinku na Sasilo wilayani Manyoni

Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Manyoni Mashariki (CCM), Dk. Pius Chaya.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji mpango wa serikali wa kufanya utafiti ili kubaini uwapo wa madini ya aina mbalimbali katika jimbo la Manyoni Mashariki kwenye kata hizo.

Akijibu swali hilo, Prof.Manya alisema matokeo ya utafiti wa awali yanaonyesha kuwa kuna viashiria vya uwapo wa dhahabu katika Kata ya Makuru. Pia alisema katika kata hiyo, kuna ulanga na kata ya Solya kuna madini ya urani, thorium na ya ujenzi.

Pia alisema kata ya Kintinku kuna madini ya urani na kata ya Sasilo hakuna viashiria vya uwapo wa madini.

"Ili kuwezesha uchimbaji kufanyika, utafiti wa kina unahitajika ili kujiridhisha na kiwango cha mashapo iwapo yanaweza kuchimbwa kwa faida au la," alisema.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alisema sekta ya madini ina mchango mkubwa kwa pato la taifa na kuitaka serikali kuja na utafiti wa kina zitakazosaidia serikali kuwekeza kwenye madini.


Ukurasa 14

Kikundi cha wanawake kilichotumia zama za corona kuibuka kiuchumi


Ukurasa 12

**ELIMU YA KUJITEGEMEA**

## Shule iliyowekeza uchumi shambani, uliojibu kwa tija ya malengo darasani

BUFE

IJUMAA FEBRUAR 12, 2021

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

BAJETI UCHUMI WA KATI

# Jicho jipya kijacho, sura mpya ya namna waletacho wafadhili

**Na Nimi Mweta**

WABUNGE na wataalamu wa uchumi wameanza kutafakari sura ya Bajeti ya Taifa katika mwaka wa fedha unaokuja, kwani kwa kalenda ya shughuli za Bunge sura ya bajeti inaletwa katika kikao cha mwezi Februari halafu inajadiliwa kwa kina zaidi katika kikao cha Aprili wabunge watoe michango muhimu kwa kina zaidi.

Inapofika mwezi Juni kabla ya Bunge kumaliza shughuli zake, ndipo inasomwa na majadiliano kumalizika kabla ya kuanza kutumika Julai Mosi. Ni tofauti na ilivyokuwa hapo awali ikitangulia kwanza.

Bunge limeambiwa hivi karibuni kuwa bajeti ijayo itakuwa na ujazo wa jumla wa shilingi trilioni 36.2, ambazo ni ongezeko la asimilia nne kutoka bajeti ya mwaka huu wa fedha, 2020/2021.

Bajeti hiyo kwa kiwango cha asilimia 72 itakusanywa kutoka vyanzo vya ndani, kuongeza nguvu ya serikali kwani mwaka huu wa fedha inakusanya na kutumia Sh. trillion 34.8 kwa makisio rasmi na inavyoelekea mchango wa nchi za nje na mashirika ya kimaendeleo utapungua kwa kiwango fulani.

Kunatazamiwa kufikia asilimia 7.9 ya mpango wa fedha kwa jumla, wakati kodi zitafikia Sh. 21.46 trillioni na mapato mengine Sh. trillioni 4.56.

Yako maeneo ambako kutakuwa na mabadiliko katika mpangilio wa bajeti na utawala wa fedha kutoka vyanzo mbalimbali na hasa kutoka mashirika ya nje au nchi wafadhili.



Kikao kimojawapo cha Bunge kilipoendelea. **PICHA: MTANDAO.**

Silio Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti, alisema akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, kuwa katika mwaka ujao wa fedha serikali haitapata fedha za kujazia bajeti kwa jumla kutoka nchi wafadhili au washirika wa maendeleo na badala yake fedha hizo zitaelekezwa moja kwa moja katika miradi husika.

Hapo inamanaisha kuwa nchi wafadhili zitatumia zaidi mashirika yasiyo ya kiserikali kutoa misaada hiyo.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo aliishauri serikali kukutana na washirika wa nchi wa maendeleo na kujadili njia mbadala za kupeleka fedha na siyo kuzielekeza katika miradi, akiainisha kuwa serikali lazima ipewe fedha hizo kuamua izielekeze wapi kwa msingi wa vipaumbele vyake.

Bila shaka sehemu isiyo ndogo ya wabunge walishangilia pendekezo hilo. Kinachoonekana hapo ni kuwa kamati inachelea mazingira ambayo wafadhili wanapeleka fedha moja kwa moja katika miradi.

Mashirika yasiyo ya kiserikali ambako fedha hizo zitapitishwa, yameandikishwa kwa mujibu wa sheria zetu na bila shaka wafadhili nao wanataka walengwa watumie fedha katika namna walivyonuia.

Inawezekana, kwa mfano kwa kamati hiyo kutoa azimio kukagua mara moja au mbili kwa mwaka maendeleo ya miradi hiyo, kulieleza Bunge.

Kuondolewa baadhi ya maeneo ya miradi ya maendeleo pale nchi wafadhili zinaipelekea fedha moja kwa moja ni kupunguza ukali wa kuchagua miradi ya kupeleka fedha za serikali na hali hiyo ikitumika vyema, inaweza kurahisisha mjadala wa vipaumbele bungeni.

Tatizo wanalopata baadhi ya wabunge ni kuwa upo muhimili mwingine wa kuchagua vipaumbele na siyo serikali na kamati za Bunge peke yao.

Ni hali inayoweka mbali au mwanya kwa upande mwingine kwa kamati za bunge kuwa kiunganishi kati ya miradi inayoendeshwa na mashirika yasiyo ya kiserikali na inayoendeshwa na taasisi za umma, iwe kioo cha aina yake na njia tofauti ya mawasiliano.

Kuna maeneo kama upatikanaji na bei za taulo za wanafunzi shuleni ambalo limekuwa likitatiza pale linapotolewa uamuzi kupitia bajeti, ndipo wazifuate dukani.

Tanzania sasa imefikia Uchumi wa Kati, hatua za mwanzo na kuna ongezeko la asimilia nne na ziada katika bajeti ijayo, huku sehemu ya fedha kutoka nje ikiwa ni mikopo inayotolewa kwa serikali, ni wazi kuwa kipande cha misaada kinacholenga mashirika huria ni kidogo tu.

Katika asilimia 7.9 ya misaada au fedha ya nje, hiyo inayokwenda katika mashirika huria kwa haraka inaweza kuwa sawa na nyongeza ya asilimia 4.0 au zaidi kidogo.

UCHUMI

ELIMU YA KUJITEGEMEA

# Shule iliyowekeza uchumi shambani, uliojibu kwa tija ya malengo darasani

- Mkakati wahamishiwa watokako watoto
- Kila mmoja ana mgomba wake nyumbani
- Foleni ya wanakijiji kufuata kilichoibuka

**Na Beatrice Philemon**

"UJAMAA na Kujitegemea Njia Sahihi ya Kujenga jamii Iliyo Sawa na Huru." Ni itikadi, msimamo wa kisiasa na mwongozo wa kiserikali uliotumika katika miaka 24 ya uongozi wa wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere.

Mwongozo huo, pia umeandaliwa angalizo la kielimu, ambalo Rais Mwalimu Nyerere, aliiweka juu ya aina ya Elimu ya Kujitegemea, ambayo hadi sasa ni sehemu ya maudhui ya Sera ya Elimu ya nchi sasa, kama inavyosomeka:

"Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea, falsafa hii imekuwa ndio msingi wa elimu Tanzania tangu mwaka 1967. Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea inaweka msisitizo katika mambo yafuatayo:

"Uwiano kati ya elimu na mahitaji ya jamii au walengwa; kukuza fikra tunduizi na tabia za udadisi; kujifunza kwa kuhusisha nadharia na vitendo; kukuza kujiamini, kufanya uamuzi na kuthamini utu; na kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali."



Mjumbe wa mradi wa Eco-School kutoka kijiji cha Msufini, Kata ya Hembeti, Shukuru Sufiani, akimkabidhi mwanafunzi wa darasa la tano, Prisca Simon, mbegu ya mgomba akapande nyumbani, ili kueneza ujuzi wa ulimaji mgomba kwenye jamii.

KINACHOFANYIKA MVOMERO

Ni ndani ya mtazamo huo hasa wa kuoanisha elimu na uzalishaji mali, ndipo Shule ya Msingi Msufini iliyoko katika Kata ya Hembeti, umbali wa kilomita 41 kutoka Mvomero mkoani Morogoro, imeanzisha miradi inayotafuta majibu ya changamoto za shule yao.

Lengo kuu ni kuibua kiwango cha taaluma na shuleni kusambaza ujuzi kwa jamii inayozunguka shule kwa maendeleo endelevu.

Tayari imeshaanzisha mradi wa kilimo cha kisasa cha migomba, ufugaji wa nyuki na uhifadhi wa mazingira kupitia mradi wa 'Eco-School Programme' unaofadhiliwa na shirika lake la Danish Outdoor Council (DOC), kutoka nchini Denmark.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Msufini, Jonas Mhoka, anasema wameamua kujikita katika ulimaji migomba, ili kuwasaidia wanafunzi chakula wawapo shule na kujiongezea kipato.

Pia, hilo ndilo linahusika na kueneza ujuzi kwa jamii inayowazunguka wajiongezee kipato kwa kuapanda mazao kama migomba.

Wanafunzi hao wa Msufini, pia wamepanda miti na nyasi shuleni kulinda baioanuai, kuzuia mmonyoko wa udongo na hairuhusiwi kuchoma taka ndani ya shule.

Lingine linatajwa kuwa ni mradi wa nyuki, kukiwapo mizinga 15 iliyokwishatundikwa na kila moja ina uwezo wa kuzalisha lita 20 za asali kwa msimu wa mavuno.

SURA YA MRADI

Mwalimu Mkuu Mhoka, anauambia ugeni uliombatana na mdau wa mradi wa Eco-School kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), ulianza kutekelezwa shule yetu mwaka 2017.

Anaorodhesha malengo ni kuboresha mazingira ya shule, kuinua taaluma, kuanzisha miradi midogo, kutatua changamoto za shule, kujiongezea kipato na kusambaza ujuzi kwa jamii jirani katika mtazamo maendeleo endelevu.

Mengine anayataja ni kuwajengea uwezo walimu, wanafunzi na jamii inayowazunguka kuhusu maarifa ya matumizi endelevu ya maliasili, ili kuboresha maisha yao.

Ni mradi unaokusudia kukuza kanuni za elimu kwa maendeleo endelevu nchini kupitia shule za msingi na unakuza ushirikiano na jamii katika matumizi endelevu ya maliasili, ikiwaongezea faida wanafunzi watokao katika shule na jamii maskini.

MIRADI ILIYOPO

Anasema shule imeshapanda miche 600 za migomba kwa ajili ya chakula cha wanafunzi, biashara na kueneza ujuzi kwa majirani, akifafanua:

"Mpaka sasa jumla ya mikungu 250 ya ndizi yenye thamani ya Sh.1,280,000 imeuzwa na ndizi hizo zilitumika kupika chakula cha wanafunzi shuleni na kiasi cha Sh. 500,000, kilichobaki kiliwekwa benki kwa ajili ya maendeleo ya shule," anasema.

Pia, Mhoka anasema wamegawa miche 250 za migomba kwa shule ya msingi jirani, Mpapa, 56 imepewa Kanisa la Anglikana; 130 Shule ya Msingi Kunke na 80 wamepewa watu binafsi.

Anasema kuna kiasi cha pesa walizopata kwa kuuza ndizi zimetumika kujenga madarasa mawili, yaliyoishia kwenye hatua ya boma, bajeti ya kumalizia ikiwa imekwama kwa sasa.

CHANGAMOTO & MAFANIKIO

Mwalimu Mkuu anasema, ingawa mradi umewasaidia kuasisi miradi mingine midogo, kuna anayoitamka: "Wateja wetu wakuu ni wazawa ambao wananunua ndizi kwa bei ndogo."

Anasema shule inataka kupanda ndizi zenye soko zaidi, malengo ni kuanzia Agosti ijayo, waweze kupata mbegu bora zaidi za migomba , ziwasaidie wanafunzi kupata chakula na zao la biashara, itakayowasaidia kutekeleza miradi ya maendeleo shuleni.

"Tunaishukuru serikali ya Denmark na TFCG kuleta programu hii katika shule yetu, kwa sababu kiwango cha elimu kimeinuka, jamii imepokea mradi vizuri na baada ya kuona mradi una manufaa kwa watoto wao shuleni ulinzi kutoka kwa wazazi umeimarika," anasema.

Manufaa mengine yanatajwa ni shule kuongeza kwa ufaulu asilimia 50 hadi 78 na kuna wanajamii jirani wanajitokeza kujifunza uhifadhi wa mazingira na kilimo cha migomba, wakaendeleze katika maeneo yao.

Pia, shule imetoa mbegu za migomba kwa wanafunzi ili waendeleze ujuzi kwenye jamii zao, pia waende kupanda kwenye maeneo yao.

Mkuu wa Shule anawaomba wadhamini, asasi ya TFCG kufuatilia miradi kwa ukaribu zaidi kama kilimo cha migomba, mihogo, mboga, upandaji miti, ufugaji nyuki katioka mtazamo endelevu.

Pia ana rai: "Walimu tuendelee kusimamia miradi hii kwa sababu inagusa maisha yao na jamii kuja kujifunza na tunaamini kupitia vikao vyao hizi taarifa zitafika kwa jamii waje."

WADAU NA WASHIRIKA

Mjumbe wa Mradi wa Eco-School, kijijini Msufini, Shukuru Sufiani, ana wito kwa walimu na wanafunzi kuungana na Kamati ya Mradi wa Eco-School ili wasonge kimaendeleo.

"Elimu niliyopata kutoka Shule ya Msingi Msufini, hivi sasa nimefanikiwa kupanda miche 30 ya migomba katika shamba langu, ili kupata mazao bora zaidi, kujiongezea kipato na watu wengine waje kujifunza toka kwangu," anasema.

Mwanafunzi wa darasa la tano, Prisca Simon, anausifu mradi 'upo vizuri'wakinufaika na mazao kama kama ndizi zinazowanaufaisha kwa mlo shuleni, ingawa kuna sura ya pili ya wakati mgumu wa soko lao.

"Pia, tunaomba taasisi za utafiti zitusaidie kupata aina nyingine ya mbegu za migomba, ambazo zinakubalika kwenye soko la ndizi," anasema Prisca.

Mwanafunzi wa darasa la sita, Kassim Shaban, anasema kupitia wanafunzi waliofundishwa jinsi ya kulima, kupanda miche ya migomba kwa kutumia utaalamu wa kisasa, kupalilia, kukagua na siku nyingine wanakula ndizi shule.

"Hapo awali hali ilikuwa mbaya, unakuta mwanafunzi mwingine anatembea umbali wa kilometa10 kuja shule na akifika shule anakuta vipindi vingine vimemalizika.

"Baadae sisi wanafunzi tunaamua kumfundisha masomo tuliyofundishwa na asipoelewa tunamwambia aende kwa mwalimu amfundishe tena na akifika kwa mwalimu anamuelekeza," anasema Kassim

Kijana huyo anataja matunda ya elimu yake, mpaka sasa amepanda miche mitatu ya migomba nyumbani kwao ambayo bado haijaanza kutoa ndizi, huku kila mwanafunzi ameambiwa apande mgomba nyumbani, katika namna ya kueneza elimu hiyo kwa jamii inayozunguka, ijiongezee kipato na kuboresha maisha.

MWEKA HAZINA

Mweka Hazina wa Kamati ya Eco-School, Zagana Mvungi, anasema mradi huo walioanzia kilimo cha migomba, umewaletea maendeleo katika jamii.

"Wakati tunaanza kutekeleza mradi huu, ilikuwa changamoto kubwa kwa sababu tulikuwa tukiwaambia wanafunzi kwenda kupalilia shamba la migomba, wazazi wao walikuwa wanatutukana, lakini wengine walikuwa waelewa na waliruhusu watoto wao kupalilia," anasema.

Mvungi anajivunia mafanikio ya ufaulu wa wanafunzi na waliopata ujuzi, hivi sasa wazazi wako mstari wa mbele kuwapa ushirikiano kwa watoto wao.

Hadi sasa, mradi huo unatekelezwa na Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG) katika shule 34 wilayani Mvomero, ukifadhiliwa na shirika la Danish Outdoor Council (DOC) la Denmark.

MIRADI VS UFAULU

Mwalimu Mkuu anafafanua uhalisia wa ufaulu, akioanisha na ujio wa mradi, akiwa na takwimu: Mwaka, 2016 walifaulu asilimia 51 ya waliofaya mtihani na mwaka 2017 walikuwa nusu ya waliofanya mtihani.

Katika awamu ya waka 2018, ambao mradi ulishaanza, wastani wa ufaulu ghafla ulipaa hadi robo tatu ya wanafunzi wote (78.2%) wasichana wakiwa juu maradufu kama kawaida yao.

Mwaka uliofuata 2019, ilifika asilimia 68 ya waliochaguliwa na mwaka jana, iliwekwa rekodi ya watahiniwa wote shuleni hapo walifaulu.

Pia, katika ufaulu huo rekodi yake wasichana katika kila mwaka iliorodheshwa kuwa juu zaidi zaidi ya mara mbili ya wavulana

Shule ya msingi Msufini ilianzishwa mwaka 1975 na hadi sasa ina wanafunzi 447, kati yao wasichana 213 na wavulana 234, walimu 10 waliosajiliwa na serikali na watano wa kujitolea.

Mpaka sasa shule ina vyumba saba vya madarasa, kati yake kimoja hakijakamilika, matundu sita ya choo, kukiwapo hitaji la vyumba vya madarasa mawili, maktaba moja, matundu 11 za choo, huku vilivyopo vikielezwa na Mwalimu Mkuu, kwamba havina ubora unaopstahili



Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Msufini, Jonas Mhoka, akiwaelekeza wanafunzi sehemu ya kusoma katika somo la mazingira. **PICHA ZOTE: BEATIRCE PHILEMONE.**

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Kulikoni kwenye sukari, saruji, mafuta?






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

BAADA ya vita vya Kagera, miaka ya baadaye ya 1980, nchi iliingia katika matatizo makubwa kiuchumi, mpaka Rais Julius Nyerere akalitangazia taifa kujiandaa kujifunga mikanda, ili kukabiliana na hali hiyo.

Tuliokuwapo tulishuhudia hali ilivyokuwa ngumu, bidhaa madukani ziliadimika, achilia mbali fedha mifukoni na wananchi kulazimika kupata bidhaa za chakula na zingine kwa mgawo.

Simulizi ni kwamba, kama safari hii mtaa ulipata bidhaa fulani, safari ijayo ni zamu ya mtaa mwingine kupata bidhaa hiyo na hata mfumo wa ununuzi ukawa kujipanga kwenye maduka ya ushirika, ambako Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC), lilipeleka bidhaa hizo kuuzwa kwa foleni.

Ni kipindi ambacho hata mtu aliposafiri nje ya nchi, zawadi ya dawa ya mswaki na sabuni, ilikuwa kubwa na yenye thamani sana, kwa sababu ni bidhaa zilizokuwa zikiuzwa kwa magendo nchini kutoka nje ya nchii. Watu walikamatwa kwa kukutwa na bidhaa za magendo.

Rais Ali Hassan Mwinyi katikati ya miaka ya 1980, aliipokea nchi katika mazonge hayo, utawala wake ukaingia katika sera mpya huria maarufu 'Ruksa' ikimruhusu kila aliyekuwa na uwezo wa kufanya biashara, kufanya hivyo kwa kuingiza bidhaa adimu nchini.

Bidhaa zikawa nyingi, suala la fedha mfukoni, likabaki la kila mtu na akili yake.

Nchi hata hivyo kwa nia njema kabisa, ikalazimika kukopa kutoka jumuiya ya kimataifa ili kunusuru uchumi wake na kuokoa maisha ya Watanzania.

Ndiyo sababu hata katika miaka ya 1990, akiipokea Rais Benjamin Mkapa, nchi ikalazimika kulipa madeni na kuingia makubaliano na mashirika ya kimataifa kuendelea kusaidia kujenga uchumi.

Katika miaka ya kati ya 2000, ilipokewa na Rais Jakaya Kikwete, nchi ilikuwa katika hali nzuri, huku ikiendelea kuagiza baadhi ya bidhaa kutoka nje ndani ya mfumo huria. Hakukuwapo matatizo ya kiuchumi kiasi cha kutisha.

Hatimaye nchi ikapokewa na Rais John Magufuli, ambaye alijitanabaisha kama mtu wa kazi na aliyedhamiria kupambana na ufisadi na kujenga uchumi, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda, huku akitamba nchi kuwa tajiri isiyohitaji utegemezi wa nje kujijenga.

Viwanda vinafufuliwa, miradi ya kimkakati inajengwa, tunatafuta kujitegemea zaidi na katika kulithibitisha hilo, tulichaguana mwaka jana kwa kutumia fedha zetu, tunajenga reli ya kisasa kwa fedha zetu na hata mradi mkubwa wa kufua umeme kwa fedha zetu wenyewe.

Lakini, ndani ya juhudi zote hizo zenye mafanikio, tunakabiliwa na matatizo yanayojitokeza tena. Mwaka jana, tulianza na upungufu wa sukari na baadaye wa saruji na sasa mafuta ya kula.

Serikali imekuwa kila ikisikia tatizo, inachukua hatua za kukabiliana nalo. Lakini kinachoshangaza, ni kwanini wenye dhamana mahsusi wasubiri mpaka hali ishike, ndipo waseme na hatua zichukuliwe?

Nadhani wenye dhamana kuu ya kwenye bidhaa tajwa, vikiwamo vyakula wanapaswa kujihoji na kutoa maelezo haraka kwa umma.

Sababu ya sukari, saruji na mafuta ya kula zinakosekane madukani na bei ipande, huku wahusika wako kimya kwanza. Watu wanaweza kujiuliza maswali yasiyopendeza kuhusu hali hiyo.

Tanzania sasa ni ya uchumi wa viwanda, wapi tunakwama kuzalisha bidhaa hizo na zingine za kutosheleza matumizi ya ndani na ziada kuuza nje?

Mbona tuna viwanda vya sukari na mashamba ya miwa? Kama havitoshi au hayatoshi, kwa nini tusijenge hata vidogo na kuongeza mashamba?

Hivi kweli hatuna malighafi ya kutosha kutengenezea saruji nchini? Mafuta ya kula nayo mpaka tuagize nje? Wakulima wa alizeti, ufuta, karanga, pamba, minazi, wakiwezeshwa tutajitosheleza kwa mafuta ya kula.

Mbona tulikuwa na viwanda vyetu vya mafuta ya kula kama vile ya TanBond na vingine vya aina hiyo, tunavikumbuka? Alamsiki!

BIASHARA

FAHARI YETU

# Kikundi cha wanawake kilichotumia zama za corona kuibuka kiuchumi

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI baadhi ya wanajamii wakiwa wamejifungia ndani kwa hofu ya kupata maambukizi ya ugonjwa wa Corona, pia kuna wengineo walitoka nje kutumia fursa hiyo kuchangamsha akili wanufaike kimaendeleo.

Ndio aina ya mawazo katika kikundi kiitwacho Fahari Yetu kinachoundwa na wanawake 11, wenye makao makuu eneo la Soko la Muslim, Tabata jijini Dar es Salaam.

Mbinu waliotumia kinamama hao waliweka hofu nyuma na kuingia mtaani kutafuta ujuzi wa kujiongozea kipato, chini ya nguzo usemi 'mtafutaji hakosi.'

Ni juhudi zilizozaa matunda baada ya kupata msaada wa uliowapa ujuzi wa kutengeneza sabuni za maji na mkaa unaotokana na taka za vifuu.



Wanakikundi cha Fahari Yetu wakiwa kazini. Chini, bidhaa yao makaa ya mawe. **PICHA ZOTE: JENIFER GILLA**

Agness Damian, mwenye umri wa miaka 50, anaeleza furaha yake kujiunga na kikundi hicho, kwani amenufaika kwa mafunzo mbalimbali, ikiwamo stadi ya kutengeneza sabuni za maji wanaziingiza sokoni, kwa wahitaji wa kutakatisha mikono kwenye ofisi mbalimbali.

Mama huyo mwenye watoto watatu anasema walikaa kama kikundi na kuziona fursa kupitia janga la ugonjwa wa corona, wakaamua kutengeneza sabuni, wakianza na kutafuta msaada wa elimu ya utengenezaji sabuni hiyo.

Baada ya kupata elimu hiyo, walitafuta masoko na kukusanya oda za wahitaji ili kupata kiwango cha uzalishaji na kutoa huduma. Anafafanua:

"Tuligawana vikundi vya watu wawili, tukawa tunazunguka kwenye ofisi kueleza biashara yetu na kukusanya oda. Mwanzo kazi ilikuwa ngumu, lakini 'tulikomaa' mpaka sasa tunakusanya oda tatu hadi nne kwa wiki za sabuni ya lita na chupa kumi za lita moja."

Katika kikundi hicho, Amina Mohamed (35), mwenye dhamana ya hifadhi ya fedha za kikundi, anaeleza bei ya bidhaa hizo ni kati ya Sh.10, 000 na Sh. 2,000 kulingana na vipimo na wanamudu kukusanya wastani wa Sh. 50,000 kutoka na mauzo yao.

MIRADI MINGINE

Kikundi pia kinatengeneza mkaa unaotokana na taka za vifuu, ikinufaisha kikundi na mwanachama mmoja mmoja. Warda Omary (42), Mwenyekiti wa Kikundi, hicho ana simulizi yake akisema:

"Nashukuru sana kupata fursa ya kujifunza kutengeneza mkaa huu, kwani unaniongezea kipato mimi binafsi kwa kuwa na utengenezaji, halafu nauza kwa wiki naweza kupata Sh. 15,000 hadi Sh. 20,000 inanisaidia na watoto."

Hata hivyo, mama huyo ambaye ni mjasiriamali wa mboga za majani anakiri mwanzo maisha yalikuwa magumu kwake, kutokana na faida ndogo ya biashara hiyo ya mkaa.

Ni kauli inayoungwa mkono na Maimuna Hassan (73), anayejivunia kikundi kuzalisha mkaa kumemwongezea kipato, hali kadhalika anautumia kupikia, hali inayompunguzia gharama za maisha.

"Zamani nilikuwa natumia mkaa wa Sh. 4000 kwa siku kutokana na ukubwa wa familia yangu na ule mkaa wa kuni kutumika mwingi, lakini huu mkaa wa taka natumia Sh.1000 tu siku nzima kwa kuwa ni mzito," anasema.

Anadokeza mpango wake ujao ni kuutumia mkaa huo kukaangia samaki wa biashara, kwani kuni anazotumia zinamdhuru kiafya.

Getrude Nestory mwenye umri wa miaka 38, anayesema pia wanatengeneza siki, bidhaa itokanayo na pilipili, huku kukiwapo mradi mwingine walio nao, ni uokotaji na uuzaji vyuma chakavu na bidhaa za plastiki.

**MALENGO YALIVYOKAA**

Amina Mohamedi (35), Mweka Hazina wa kikundi anasema wanakoangaza sasa ni kumiliki miradi mikubwa zaidi.

Anaeleza utaratibu wao ni kukutana kila wiki kwa ajili ya kutengeneza mkaa wanazouza na makusanyo yake yanapangiwa malengo kwa ajili ya mambo ya maendeleo.

"Kwa wiki tunatengeneza mkaa kilo 20 hadi 40 ambao tunauza kilo Sh. 1000 ambayo hutupatia si chini ya Sh.20,000 tunayoiweka benki," anasema Amina.

Anasema, zao la makusanyo ya mwaka jana walinunua shamba la ekari moja eneo la Kisemvule wilayani Mkuranga kwa gharama ya Sh. milioni nne na mwaka mpya wameanza na akiba ya Sh. 400,000.

**CHANGAMOTO**

Kila jambo zuri halikosi changamoto. Wanakikundi hao wanalalamikia vitendea kazi kuwa vichache, hivyo inarudisha nyuma kasi yao ya utengenezaji mkaa na sabuni.

Mwenyekiti wa kikundi hicho, Warda, anataja upungufu katika mashine za kutoa, kuchanganya na kusaga mkaa ni kikwazo kwao katika uzalishaji, anapiga mbiu kwa wadau wasaidiwe kusonga mbele.

**WADAU WASIMAMIZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Forum CC, inayowasimamia kinamama hao wa Tabata, Rebeca Muna, anasema Furaha Yetu imo katika vikundi vitatu wilayani Ilala vilivyopata fursa ya kutembelewa nao na kupewa mafunzo pamoja na fursa za ujasiriamali.

"Tumewafundisha jinsi ya kutengeneza mkaa kupitia taka hasa za vifuu, kuuza vyuma chakavu na chupa za plastiki, hii yote ni katika kuhamasisha utunzaji wa mazingira na kuepuka athari za mabadiliko ya tabianchi, pia tumewafundisha kutengeneza sabuni," anasema Rebecca, anayesema bado wameshikamana katika harakati hizo kuwasaidia.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Msimbazi, Tabata jijini Dar es Salaam, Godfrey Anthony, anaeleza kufurahishwa kuwapo vikundi vya kinamama vilivyo katika juhudi za maendeleo, kutafuta hatua ya kusonga zaidi.

Anawakumbusha kwamba asilimia 10 ya makusanyo ya mapato katika kila halmashauri inarudishwa kwa jamii na asilimia nne huenda kwa kinamama kwa njia ya mikopo isiyokuwa na riba, hivyo anawasahauri wanawake wasibweteke, waunde vikundi vya maendeleo wakopeshwe.

**WALIKOTOKEA**

Mwenyekiti wa FahariYetu, Warda, anakumbusha walikotokea, kwamba kikundi kiliundwa mwaka 2019 na ndipo walipotembelewa na taasisi ya Forum CC ya Dar es Salaam.

Ni hatua iliyowapa fursa ya kufunzwa umuhimu na namna ya kutunza mazingira na ndio waliowaongoza katika kutengeneza mkaa utokanao na taka na elimu ya ujasiriamali wake, uliozaa matunda.

"Mkaa huu mimi nautumia katika biashara yangu ya mama ntilie na unanirahisishia gharama kwa kuwa huu unatumika kidogo, ukilinganisha na wa kawaida, ukiuweka katika jiko unapikia maharage mpaka yanaiva bila kuongeza" anasema.





# Mbaroni madai kuua mtoto kwa fimbo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU 10 wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma mbalimbali akiwemo kijana Ahadi Angetile (18) mkazi wa Kijiji cha Mpunguti wilayani Rungwe anayedaiwa kumuua mtoto Prosper Paradiso (5) kwa kutumia fimbo.

Akizungumza na wandishi wa habari jana, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema tukio la mauaji hayo lilitokea Februari 9, mwaka huu, saa 6:00 mchana.

Alisema mtuhumiwa ambaye ni baba mdogo wa marehemu, alimshambulia mtoto huyo kwa kumpiga na fimbo maeneo ya kichwani na tumboni mpaka kumsababishia kifo.

**Kwa mujibu wa sheria kosa la kusafirisha binadamu ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni kali na vyombo vinavyotumika kuwasafirisha binadamu hao hutaifishwa kwa mujibu wa sheria.**

"Kwa mujibu wa taarifa za wanafamilia ni kwamba kijana huyo ana matatizo ya akili lakini chanzo cha tukio hilo ni kwamba mtuhumiwa alitukanwa na marehemu ndipo akashikwa na hasira na kuanza kumchapa na fimbo mpaka akamuua," alisema Matei.

Katika tukio la pili, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia wahamiaji haramu saba raia wa Ethiopia kwa kosa la kuingia nchini bila kuwa na vibali kinyume cha sheria huku pia likiwakamata madereva wawili waliokuwa wanawasafirisha.

Kamanda Matei alisema watu hao walikamatwa Februari 9, mwaka huu, saa 8:00 mchana katika Kijiji cha Changarawe wilayani Chunya baada ya askari waliokuwa doria kupata taarifa za siri kuwa kuna gari linasafirisha raia wa kigeni.

Alisema baada ya kupata taarifa hizo, waliamua kuweka kizuizi katika eneo hilo na ndipo wakalikamata gari aina ya Toyota Noah lenye namba za usajili T.257 DAY lililokuwa linaendeshwa na madereva wawili, Christopher Masese (37) na Khalfan Khatibu (34) wote wakazi wa jiji la Mwanza.

Baada ya askari kulipekua gari hilo walibaini kuwa ilikuwa imewabeba raia hao saba wa Ethiopia ambao mmoja wao anajulikana kwa jina la BdasaloTesef (27).

"Tunaendelea kuwahoji madereva hao waliokuwa wanawasafirisha wahamiaji hao ili kuendelea kubaini mtandao mzima wa mawakala wa biashara hii haramu ya kusafirisha binadamu," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka madereva wa vyombo vya moto kuacha tabia hiyo ya kuwasafirisha wahamiaji haramu kwa maelezo kuwa ni kinyume na sheria za kimataifa pamoja na maadili ya dini mbalimbali.

Alisema kwa mujibu wa sheria kosa la kusafirisha binadamu ni kosa la jinai ambalo adhabu yake ni kali na vyombo vinavyotumika kuwasafirisha binadamu hao hutaifishwa kwa mujibu wa sheria.

Januari 13, mwaka huu, wahamiaji haramu wengine 61 walikamatwa na jeshi hilo katika kijiji cha Garijembe wilayani Mbeya wakisafirishwa kwenye lori huku afya zao zikiwa zimezorota kutokana na kukosa chakula kwa muda mrefu.

## Wafugaji waomba maeneo ya kuchungia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WAFUGAJI wa Kijiji cha Kimondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wameiomba serikali iwapatie maeneo ya kuchungia mifugo yao kwa madai kuwa waliyokuwa wanayatumia awali yalichukuliwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA).

Walitoa ombi hilo juzi walipokuwa wanakabidhiwa dawa za kuogesha mifugo zilizotolewa bure na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwenye josho la kijiji hicho ikiwa ni mikakati ya serikali kuwasaidia wananchi kuboresha mifugo yao. Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Subi Njate, alisema kijiji hicho kwa sasa hakina eneo lolote la kuchungia na hivyo wafugaji wanalazimika kuchungia kwenye maeneo madogo yaliyomo pembezoni mwa mashamba.

Alisema hali hiyo inasababisha migogoro ya mara kwa mara na wakulima kutokana na mifugo kula mazao ya wakulima na kwamba hawawezi tena kuchungia kwenye eneo lao la awali kwa sababu sheria zinazuia.

"Tunamuomba Rais Magufuli kama anatusikia atusaidie tupate maeneo ya kuchungia mifugo yetu maana tunapata shida sana, sasa hivi tunapishana sana na wakulima kwenye mashamba yao," alisema Njate.

Aliishukuru Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuwasaidia dawa hizo za kuogesha mifugo kwa maelezo kuwa zina faida kubwa kwa wafugaji ikiwemo kuboresha mifugo na kuongeza tija.

Baadhi ya wafugaji wa Kijiji hicho, walisema tangu erikali ilipoanza kuwapatia dawa hizo wamepata manufaa makubwa kutokana na mifugo yao kuwa na afya njema na kuongeza kasi ya kuzaliana tofauti na ilivyokuwa awali.




Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkomora (wa pili kulia), akionyesha kitabu cha mpango shirikishi wa usimamizi wa rasilimali za maji katika Bonde la Ziwa Rukwa, baada ya kukizindua katika jukwaa la wadau wa rasilimali za maji katika bonde hilo, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Watakiwa kusimamia matumizi bora ardhi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imezishauri mamlaka za maji na mabonde katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kusimamia kikamilifu matumizi bora ya ardhi ili kuepusha migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

Wito huo ulitolewa jana na Kaimu Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Mwajabu Nyamkomora, wakati wa kikao cha Jukwaa la Wadau wa Sekta ya Maji Bonde la Ziwa Rukwa ambacho kinafanyika jijini Mbeya.

Alisema matumizi bora ya ardhi yatasaidia kuondoa migogoro na uvamizi wa vyanzo vya maji kwa sababu kutakuwa na maeneo maalum ya kufanyia shughuli hizo bila kuathiri mazingira.

"Moja ya mikakati inayotakiwa kufanywa na jukwaa hili ni kwenda kuelimisha matumizi bora ya ardhi wa wananchi itasaidia kila mmoja kupata eneo lake la kufanya shughuli zake. Ukuaji wa miji na maendeleo mengine yanachochea uvamizi kwenye vyanzo vya maji na kuharibu," alisema Nyamkomora.

Alishauri wachimbaji wa madini kuwa makini na shughuli zao kwa kuzingatia kanuni na sheria za utunzaji mazingira hasa kutoka kemikali kwenye vyanzo vya maji.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Wadau wa Mabonde Taifa, Mhandisi Mbogo Futakamba, alisema maji ni sawa na moyo wa mwanadamu hivyo kunahitajika umakini mkubwa kuyatunza.

Alisema maji yanapaswa kutunzwa kwa kuhakikisha kila mwananchi anahifadhi na kutunza vyanzo vya maji kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha sasa na baadae.

Mkurugenzi wa Bonde la Ziwa Rukwa, Mhandisi Grace Chitandam alisema Jukwaa la Watumia Maji katka bonde hilo limekuwa na mchango mkubwa katika kukabiliana na uharibifu wa vyanzo vya maji.

Alisema miongoni mwa wadau wanaliosaidia kukabiliana na uharibifu wa vyanzo vya maji ni Jumuiya za watumia maji kutoka Mikoa ya Nyanda za juu kusini kwa kusimamia na kulinda vyanzo vya maji kwa mujibu wa sheria.

Alisema jumuiya ya watumia maji imesaidia kulinda na kutunza vyanzo vya maji hasa kwa mito na mabonde yaliyokuwa yanakauka kipindi cha kiangazi sasa yanatiririsha maji kwa kipindi chote cha mwaka.



# Waziri atangazia kiama waliotelekeza ranchi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ametoa siku nne kwa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO) kuwanyang'anya watu wote walioshindwa kuendeleza vitalu walivyokodishwa kwa kuwa wamekiuka masharti ya mkataba.

Pia amewataka baadhi ya wananchi wanaoishi karibu na ranchi na waliovamia maeneo hayo waondoke kwa hiari kabla ya kuondolewa kwa nguvu.

Waziri Ndaki alitoa agizo hilo juzi alipokuwa akizungumza na viongozi wa Chama cha Wafugaji katika kikao cha kujadili maendeleo ya sekta ya mifugo kilichofanyika jijini hapa.

Alisema kuna watu wengi wamekodishwa maeneo katika ranchi lakini wameyatelekeza na wengine wamekodisha watu wengine kinyume cha makubaliano.

**Maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupumzishia mifugo yatapunguza ili wapewe NARCO na kuyakodisha kwa wafugaji.**

"Ifikapo Februari 15, mwaka huu, wale wote waliochukua vitalu na wamekodisha watu wengine wanyang'anywe maeneo hayo na hatutajali mikataba yao kwani wameshakiuka masharti na baada ya kupita muda huo, waanze kusakwa wote waliochukua maeneo hayo na kuwanyang'anya ili wapewe wafugaji makini kutumia maeneo hayo kuweka mifugo yao," alisema.

Ndaki alisisitiza kuwa wameanza mikakati ya kuiweka vizuri NARCO ili maeneo makubwa iliyo nayo ambayo mengine hawayatumii vizuri yagawiwe kwa wafugaji watakayoyatumia kufanya ufugaji wa kisasa na hatua waliyoanza ni kupunguza bei ya kukodisha vitalu.

Hata hivyo, alisema wamekubaliana kuwa bei ya kukodisha kitalu iwe ni Sh.3,500 kwa ekari moja na si zaidi ya hapo.

"NARCO inatakiwa katika yale maeneo waliyoyatenga kwa ajili ya ukodishaji. Watenge asilimia 30 kwa ajili ya kuwakodisha wafugaji wanaoishi karibu na maeneo ya ranchi hizo ili kupunguza migogoro na uvamizi wa maeneo hayo," alisema.

Pia alisema maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kupumzishia mifugo yatapunguza ili wapewe NARCO na kuyakodisha kwa wafugaji.

"Tunaamua kufanya haya ili kutibu tatizo la malisho na wafugaji waondokane na kutangatanga,"alisema.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NARCO, Paul Kimiti, alitangaza kuwa ekari moja ya kitalu katika ranchi hizo itakodishwa kwa Sh. 3,500.




Ofisa Habari wa Idara ya Habari Maelezo, Casmir Ndambalilo, akifungua kikao cha majadiliano ya pamoja na waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali, kuhusu kuvunja ukimya kwenye vyombo vya habari kwa masuala ya ukatili wa kijinsia, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Meneja Mipango wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA), Sylivia Daulinge na Meneja wa Majadiliano hayo, Aneth Andrew. **PICHA: PETER MKWAVILA**

## Shirika lajitosa kulinda korongo

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

WAKAZI wa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma wametakiwa kuacha kuwinda na kuwaua ndege aina ya korongo weupe badala yake watunze mazingira ili kuongeza idadi ya ndege hao nchini.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi wa Shirika lisilo la kiserikali la Nature Tanzania, Emmanuel Mgimwa, wakati akitambulisha mradi wa miaka mitatu wa uhifadhi ndege katika Wilaya ya Kongwa.

Mgimwa alisema lengo la kuleta mradi huo Dodoma ni kutaka kuielimisha jamii katika eneo hilo na maeneo mengine mkoani hapa kuacha kuwinda ndege hao na badala yake wawatengenezee mazingira ya kuwavutia ili waendelee kuongezeka.

"Naamini mtakuwa mmeipata elimu na umuhimu wa Ndege hawa hapa nchini, wanakuja kipindi cha msimu wa chakula, ambapo husaidia kula wadudu waharibifu wa mazao," alisema Mgimwa.

Alisema ndege hao hupendelea kuja barani Afrika kipindi cha mavuno na baadae kurejea barani Ulaya, hivyo wanapowasili jamii inapaswa kuwaangalia na kuwatengenezea namna ya kuwavutia ili waendelee kuzaliana wakiwa nchini.

Pia Mgimwa alisema ndege hao wana faida kubwa hapa nchini kwa sababu husaidia kula wadudu shambani ambao mara kwa mara husumbua katika uharibifu wa mazao ya mashambani. Naye Ofisa Mradi Uhifadhi wa Nature Tanzania, Modester Kwana, alisema jamii inapaswa kulinda maliasili hizo ili kuhakikisha ndege hao wanaendelea kuwapo nchini.

# Waziri Ndugulile ataka Posta kufumuliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, amesema ipo haja sasa serikali kufanya mapitio makubwa ya sheria inayolisimamia Shirika la Posta Tanzania (TPC) ili liendane na wakati uliopo.

Dk. Ndugulile alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipokuwa akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Shirika la Posta.

Alisema sheria hiyo imekuwa ya zamani kiasi ambacho haiendani na mazingira ya sasa, hivyo kuna haja ya kufanyika mapitio makubwa ili kuirekebisha.

"Tayari nilishaagiza kufanyika kwa marekebisho madogo ya sheria hii lakini ipo haja sasa tuone ni kwa namna gani tunafanya mapitio makubwa ya sheria hii ili iendane na mazingira ya wakati tulio nao sasa," alisema Dk. Ndugulile

Vile vile, alisema sera inayotumiwa na shirika hilo hivi sasa imepitiwa na wakati na inahitaji kufaniwa marekebisho makubwa.

"Sera yetu imekuwa ya zamani sana. Hivi sasa kuna mapitio ya marekebisho ambayo yanafanywa na tunataka ikikamilika iendane na mazingira tuliyo nayo," alisema.

Kadhalika, aliliagiza shirika hilo kuboresha kitengo cha utafiti, masoko na ubunifu ili kuliondoa katika kujiendesha kwa hasara huku akisisitiza kuwa anataka kuona shirika hilo linabadilika na kuacha kufanya kazi kwa mazoea kwa kuwa wabunifu, ili kubuni bidhaa ambazo zinaendana na wakati uliopo sasa.

"Katika nafasi yangu sitegemei kuona shirika hili linajiendesha kwa hasara lazima muwe wabunifu tusisubirie kuuza stempu pekee bali tufikirie na bidhaa nyingine zinazo hitajika sasa, lazima tufanye utafaiti kuona jamii inataka nini katika mazingira ya sasa na tuachane na bidhaa zile za analojia" alisema.

Dk. Ndugulile alisema anataka kuona shirika hilo linaongeza kiasi cha ukusanyi wa mapato yake pamoja na kuongeza kiwango cha gawio kwa serikali tofauti na kipindi cha nyuma.

"Mimi kama waziri sitegemei kufanya kazi za Postamasta wa mkoa. Nikiona hali imefikia hapo nakuja kukubandua huko huko uliko. Siwezi kuvumilia mtu kufanya kazi kwa mazoea lazima tubadilike twende kidijitali na kama kuna mtu hawezi basi aondoke" alisema.

Katika hatua nyingine, Dk. Ndugulile aliliagiza Baraza la Wafanyakazi wa Posta kuhakikisha linafanya mabadiliko katika muundo wake ili kuboresha utendaji.

"Muundo wa shirika la Posta haujakaa sawa lazima tuwe na muundo rafiki utakaorahisisha kazi na si kama ilivyo sasa. Kuna watu wamepewa mamlaka lakini hawana kitu cha kufanya. Kuna mapostamasta wa mikoa hawana uwezo wa kutoa uamuzi hata wa kununua karatasi," alisisitiza.

Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta, Mwenyekiti wa Baraza hilo, Hassan Mwang'ombe, alisema watahakikisha wanafanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na waziri ili kuongeza tija katika utendaji.



# Maimamu waishtaki Bodi Udhibiti Vileo

**Na Mwandishi Wetu**

JUMUIYA ya Maimamu Zanzibar (JUMAZA) imefungua kesi dhidi ya Bodi ya Udhibiti na ushauri ya Vileo Zanzibar, baada ya kutoa vibali kwa kampuni nane za uingizaji badala ya tatu kinyume cha sheria namba 9 ya mwaka 2020.

Wakili wa Jumuiya hiyo kutoka kampuni ya (Mohas law and advocates Chamber), Omar Sheha Omar, alisema indhari ya kuishtaki bodi ya udhibiti na ushauri wa vileo imewasilishwa kwa Katibu Mkuu kiongozi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar kuanzia Febuari 8, mwaka huu.

Alisema kwamba Jumuiya ya Maimamu imeamua kufungua mashtaka baada ya kifungu cha 28(k) na 33(1) kuvunjwa baada ya kampuni nane zinazoingiza vileo Zanzibar kupewa vibali vya kuingiza pombe kinyume cha sheria.

**Kibali cha kuingiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo vya muingizaji awe ni mzanzibari, awe ni mlipa kodi, awe na ghala, magari ya kusambazia vinjwaji.**

"Kibali cha kuingiza kitatolewa kwa waingizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo vya muingizaji awe ni mzanzibari, awe ni mlipa kodi, awe na ghala, magari ya kusambazia vinjwaji,"alisema Wakili Omar akinukuu kifungu cha 33(1) cha sheria ya vileo namba 9 ya mwaka 2020.

Alisema lengo la kufuta sheria ya vileo sura ya 163 ya mwaka 1928 na kutunga sheria inayoweka masharti ya kudhibiti na kusimamia uagizaji, uhifadhi, uzaji, usambazaji ilikua na kudhibiti biashara ya vileo Zanzibar baada ya kujitokeza malalamiko mengi kutoka kwa wananchi.

Alidai Bodi ya vileo Zanzibar imeshindwa kuheshimu kifungu cha 28(k) kinachoweka sharti baa ipewe kibali ikiwa umbali na maeneo ya huduma za jamii kwa mita 1000 pasiwe na shule, kituo cha afya, msikiti, kanisa, madrasa, soko au kituo cha daladala.

"Kesi hii tunatarajia kuifungua kwa kutumia hati ya dharura kutokana na umuhimu wake baada ya kujiridhisha kwa bodi ya udhibiti na ushauri wa vileo Zanzibar imevunja sheria kwa kuruhusu kampuni nane kuingiza pombe Zanzibar badala ya kampuni tatu kinyume cha sheria," alisema wakili huyo.

Omar alisema ushahidi umeshakamilika ikiwamo kuzitambua kampuni zilizopewa vibali vya kuingiza pombe Zanzibar kinyume cha sheria pamoja na baa zilizopewa vibali vya kuendesha biashara hiyo, zingine zikiwa karibu na nyumba za ibada na shule.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maimamu Zanzibar, Khamis Yussuf Khamis, alisema kabla ya sheria hiyo kupitishwa na kusaini wa Rais wa Zanzibar, wadau walishirikishwa wakiwamo wa sekta ya vileo na kufikia muafaka kampuni za kuingiza vileo kupunguzwa na kubakia tatu.

"Sheria hii ilijadiliwa katika Baraza la Mawaziri wakiongozwa na Rais kabla ya kupitishwa Baraza la Wawakilishi na kusainiwa kuwa sheria, na Rais wa Zanzibar Mei 11,2020... inakuaje leo Bodi ya vileo imeamua kufanya maamuzi bila kufuata sheria kinyume na malengo ya kutungwa sharia?"alihoji.

Alieleza kuwa kampuni zote zilizopewa vibali za kuingiza pombe baada ya kampuni tatu kushinda zabuni zinatoa huduma kinyume cha sheria na kutaka bodi kusimamia sheria kwa vitendo ili kuondosha migongano inayojitokeza.

Kwa upande wake, wakizungumzia mgogoro huo baadhi ya wajumbe walioshiriki kutunga sheria hiyo, walisema wamesikitishwa na kitendo cha bodi kufanya maamuzi yanayokwenda kinyume cha malengo ya kutungwa sheria mpya ya udhibiti na usimamizi wa vileo Zanzibar.

"Hakuna mtu au taasisi yoyote inayokua juu ya sheria haiwezekani sheria iwekwe kando na kufanya maamuzi yanayokwenda kinyume cha misingi ya katiba na sharia,"alisema aliekuwa Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub.

Hata hivyo, Mwenyekiti wa Bodi wa udhibiti na ushauri wa vileo, Abdulrazak Abdulkadir, alisema wameamua kuweka sheria kando ili kulinda maslahi ya mapato ya Serikali, kuongeza idadi ya kampuni za kuingiza pombe kufikia nane badala ya tatu kinyume cha sheria.

## SMZ yafafanua shule zenye masharti magumu udahili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema zipo baadhi ya Shule zinaweka masharti magumu kwa watoto kujiunga nazo.

Imesema lengo si kuwanyima wanafunzi haki ya kujiunga ila ni kuangalia uwezo wao wa ufahamu ili wanafunzi wapate maendeleo mazuri.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Wizara hiyo, Simai Muhammed Said, wakati akijibu suali aliloulizwa na Mwakilishi wa Viti Maalum, Mwanaidi Kassim, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi.

Mwakilishi huyo alitaka kujua Serikali inautaratibu gani wa kuzifuatilia na kuzikagua shule hizo.

Waziri huyo alisema kesi hizo zinapojitokeza Wizara ya Elimu huzungumza na wamiliki na walimu wakuu kuondoa kasoro hizo na wizara yake ina utaratibu wa kuzikagua shule zote binafsi kila mwaka.

Aidha, Simai alikiri kuwa baadhi ya shule binafsi ada yao inapangwa kulinganisha na fedha za marekeni na shule zenye utaratibu huo ni zile za kimataifa.

Alieleza mzazi anaemuandikisha mtoto wake katika shule hizo ni uamuzi wake mwenyewe wa kukubaliana na utaratibu unaotumika, ikiwamo malipo ya ada ya masomo kwa fedha za kigeni.

Hata hivyo, alisema Serikali haina taarifa za wazazi kutozwa faini kwa sababu ya kuchelewa kulipia ada za masomo.

"Gharama za shule zinazolipwa ni zile ambazo zimeorodheshwa kwenye mkataba kati ya shule na mzazi,"alisema.



Mwakilishi wa Jimbo la Mweza, Mihayo Juma Nhunga (kulia) na Mwakilishi wa Jimbo la Micheweni, Shamata Shaame Khamis, wakifuatilia taarifa zilizokuwa zikitolewa na Spika wa Baraza la Wawakilishi katika kikao cha baraza hilo, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Wavuvi wadogo kuwezeshwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Abdaala Kombo, amesema Serikali ina mpango wa kuendeleza wavuvi wadogo, wakiwamo wa Kojani kufikia uvuvi wa kati na kwenye maji ya kina kirefu.

Katika kufanya hivyo, serikali itawapa mafunzo na kuwaunganisha na taasisi za kifedha ili kupatiwa mikopo.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na Mwakilishi wa Jimbo Kojani, Hassan Hamad Omar, aliyetaka kujua Serikali ina mpango gani katika kuwaendeleza wavuvi.

Waziri huyo alisema Wizara yake imeshafanya mazungumzo na taasisi za kifedha kwa ajili ya kuwapatia mikopo wavuvi.

"Serikali ina mpango wa kuwapatia taaluma wavuvi wadogo wa Zanzibar wanaovua uvuvi wa asili ili kuwaendeleza kufikia uchumi wa buluu," alisema Waziri huyo.

Aidha, alisema Serikali imekamilisha ujenzi wa vyuo vya elimu ya ufundi huko Mtabwe Pemba na Makunduchi Unguja ambavyo vitaoa taaluma ya uvuvi.

Pia, alisema Idara ya maendeleo ya uvuvi imeunda kitengo kitachoshughulikia uvuvi wa kienyeji kwa ajili ya kuwapatia elimu wavuvi.

"Mheshimiwa Spika, Wizara ina miradi ya kutunza mazingira ya bahari na pia ina mipango ya kuwaendeleza wavuvi kitaaluma na kuwawezesha kupata mikopo," alisema.

# Wananchi kuunganishwa maji ya bomba nchi nzima

**Na Godfrey Mushi, DODOMA**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema serikali inakuja na bei elekezi ya 'pamoja' ya kuwaunganishia wananchi maji ya bomba nchi nzima.

Amesema hatua hiyo ni baada ya kupokea malalamiko ya wananchi wengi kuhusu kuwapo kwa bei ya kuruka ya kuunganisha huduma hiyo.

Kutokana na malalamiko hayo, Majaliwa amesema Wizara ya Maji, inaendelea na utaratibu wa kuona namna inavyoweza kuwa na kiwango kimoja kwa nchi nzima ili kila mtu apate maji, kama ambavyo serikali imefanya kwenye utaratibu wa kuunganisha umeme kupitia Wakala wa Umeme Vijijini (REA), ambako wananchi hulipa Sh. 27,000.

Alikuwa akijibu swali la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei, aliyemuuliza katika kipindi cha Maswali ya Papo kwa Papo kwa Waziri Mkuu.

Dk. Kimei alitaka kujua kama serikali haioni umuhimu wa kuzingatia kwamba maji ni uhai na hitaji kubwa sana kwa kila mtu duniani, hivyo kwa nini serikali isiweke utaratibu kama wa REA wa kuweka gharama ya kumuunganishia mtu maji.

"Natambua yako malalamiko ya bei ambayo pia hata wakati tulipofanya ziara tumeona baadhi ya maeneo bei zinatofautiana na maeneo mengine. Lakini Wizara ya Maji inaendelea na utaratibu wa kuona, kama tunaweza kuwa na kiwango kimoja nchi nzima kama vile ambavyo tumefanya kwenye REA kulipa Sh. 27, 000 ili kila mtu apate maji.

"Hivi sasa kazi hiyo inakamilika na ikishakamilika Wizara ya Maji itakuja hapa itatuambia sasa uvutaji wa maji kutoka kwenye chanzo au mahali ambapo unaweza kuunganisha kuleta nyumbani ni kiasi gani.

"Kwa hiyo sera itakapokamilika na kiwango cha maji kupatikana kwa wingi, sasa tutakuja kuweka kiwango kwa kila mmoja kuvuta maji kupeleka nyumbani kwake na huo ndio mkakati wa serikali kwa sasa," alisema.

Aidha, Waziri Mkuu alisema nchi inapokuwa na maji mengi, serikali inatamani kila mmoja avute bomba apeleke nyumbani kwake, na kwa sasa inajenga vituo ili wananchi wote waweze kwenda hapo kwa ajili ya kupata maji.

Dk. Kimei wakati anamuuliza Waziri Mkuu swali hilo, alisema kwa vile serikali iliona umuhimu wa kuwafikishia wananchi vijijini umeme kwa bei nafuu, kwa kuweka utaratibu wa kumuunganishia mtu nyumba umeme kwa Sh. 27, 000.

Dk. Kimei akauliza: "Je, serikali haioni umuhimu kwa kuzingatia maji ni uhai na hitaji kubwa sana kwa kila mtu hapa duniani kuhakikisha wanaweka utaratibu kama huu wa kuweka gharama ya kumuunganishia mtu maji.

"Kwa sababu sasa hivi, baadhi ya mamlaka za maji zinatoza Sh. 350,000 hadi 600,000 kumuunganishia mtu maji. Je, mtu ataweza kweli kuunganisha maji maana kuna baadhi wameanza kunywa maji ya mifereji?"



Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, Khamisi Hamza Khamisi (kulia), akimsikiliza Gladnes Munuo (kushoto), kutoka Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA), nje ya ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasiopeleka michango Mfuko wa Fidia kukiona

**Na Ashton Balaigwa, MOROGORO**

SERIKALI imesema kuanzia sasa itawachukulia hatua waajiri wote watakaofanya ujanjaujanja na kushindwa kuwasilisha kwa wakati michango wanayoikata kutoka kwa wafanyakazi wao ili ipelekwe kwenye Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF).

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira na Vijana), Patrobas Katambi, wakati akizindua Baraza la Pili la Wafanyakazi mjini Morogoro.

Alisema katika siku za hivi karibuni baadhi ya waajiri wamekuwa wakitumia njia za ujanjaujanja kukaidi kuwasilisha makato ya wafanyakazi wao, hivyo kuanzia sasa watashughulikiwa kikamilifu.

"Niwatumie salamu hao waajiri wanaotumia ujanjaujanja kukata pesa za wafanyakazi wao halafu wanashindwa kuziwasilisha kwa wakati kisha wengine wanazifuta kampuni zao," alisema.

Alisema mfuko huo ni moja ya mifuko ambayo serikali inatambua mchango wake katika kukuza uchumi kwani unahakikisha nguvu kazi za wafanyakazi wanaougua au kuumia kutokana na kazi haipotei kupitia huduma za matibabu zinazotolewa kwa waathirika.

"Serikali inatambua mchango wenu kama mfuko wa WCF katika kupunguza madhara ya kiuchumi na kijamii yanayotokana na ajali kazini, hivyo tunaupongeza sana kwa kuendelea kuunga mkono azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda," alisema Katambi.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko huo, Masha Mshomba, alisema katika kipindi cha miaka sita ya uhai wa mfuko, kumekuwapo na mafanikio kadhaa chini ya wafanyakazi 129 ambao wameweza kutekeleza vema majukumu yao.

# Tanzania, Marekani zaboresha afya kaya maskini

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amezindua mpango mpya wa kusambaza kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii kaya maskini kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na ubalozi wa Marekani, TAMISEMI imezindua kadi za Mfuko wa Afya ya Jamii iliyoboreshwa (iCHF) (improved) Tiba kwa Kadi (iTIKA) kwa ajili ya kusaidia kaya zilizo katika mazingira hatarishi.

Taarifa ilisema katika kuzifikia kaya hizo, TAMISEMI ilishirikiana na Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID) na mpango wa Rais wa nchi hiyo wa kupambana na Ukimwi (PEPFAR) kupitia mradi wao wa kizazi kipya ambao unasaidia yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi.

Ilisema kadi za bima ya afya za iCHF/iTIKA zitagharamia huduma za jumla za afya pamoja na za watoto ambapo mradi wa USAID kizazi kipya umefadhili mwaka wa kwanza wa malipo yenye thamani ya Sh. bilioni 4.7.

"Hilo lilifanyika ili kuhakikisha kuwa watu walio katika mazingira hatarishi wanaweza kulipia malipo ya kawaida katika miaka inayofuata. Pia USAID husaidia kaya hizo kuongeza mapato yao kwa kuzisaidia kuanzisha biashara na vikundi vya kuweka akiba na kukopa.

"USAID kazi mpya itatumia mitandao yake kutoa kadi za iCHF /iTIKA kwa kaya takriban 93,000 zilizo katika mazingira hatarishi na kwa jumla ya watu zaidi ya 360,000 pia kaya zitakazofadhiliwa zitatoka katika halmashauri 85 katika mikoa 25 iliyopo nchini," ilifafanua.



# GUARDIOLA

## AISIFIA CITY KUWEKA REKODI

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola ameonyesha fahari yake baada ya Manchester City kuweka historia ya ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Swansea City na kufuzu robo fainali ya Kombe la FA.

Vinara hao wa Ligi Kuu England, wameweka rekodi ya kucheza jumla ya mechi 15 mfululizo bila kupoteza.

City imeipiku rekodi ya kushinda 14 mfululizo iliyowekwa na Preston and North End msimu wa 1891-92 na Arsenal mwaka 1987.

Kyle Walker alianza kufunga bao la kwanza kabla ya Raheem Sterling kufunga la pili na bao lake la 12 msimu huu kipindi cha pili na Gabriel Jesus akafunga la tatu.

Morgan Whittaker alifunga la kufutia machozi wakati City ikimpoteza Rodri aliyetolewa nje baada ya kuumia.

Baada ya mchezo huo, kocha huyo wa City alikuwa na furaha kubwa kuhusu kikosi chake na kuwasifia vijana wake.

Alipoulizwa kuhusu kuweka rekodi, kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich alisema: "Ni ujumbe kwa sisi wenyewe. Tumekuja kushinda, hilo lilikuwa jambo la msingi zaidi.

"Hatuwezi kukataa namna gani tumefurahishwa na kujisikia fahari kubwa kwa kuweka rekodi hii ambayo imekaa kwa muda mrefu. Rekodi zipo kwa ajili ya kuzivunja.

"Sio kazi rahisi katika zama za soka la kisasa kucheza mechi 15 na kushinda mfululizo. Tuna furaha kwa klabu yetu."



## PATO ATAKIWA LIGI KUU MAREKANI

**ORLANDO CITY, Marekani**

KLABU ya Orlando City inayoshiriki Ligi Kuu Marekani (MLS), imeweka ofa yake rasmi kwa ajili ya kumsajili mchezaji wa zamani wa AC Milan na Chelsea, Alexandre Pato.

Mshambuliaji huyo wa Brazil mwenye umri wa miaka 31 kwa sasa ni mchezaji huru baada ya kumaliza mkataba wake na Sao Paulo na sasa timu hiyo kutoka MLS inavutiwa kumsajili.

Msimu wa soka la Ligi Kuu kwa mwaka 2021 unatarajiwa kuanza ifikapo Aprili na Orlando City wametoa dau baada Sao Paulo kuchelewa kutuma dau kwa Pato ambaye kwa sasa hana klabu baada ya kumaliza mkataba Agosti 21, 2020.

Endapo Orlando City watafanikiwa kumsajili Pato watakuwa wameongeza nguvu kubwa itakayo wasaidia katika msimu mpya wa MLS unaotarajiwa kuanza mapema mwaka huu.

Kutoka katika vyanzo vya karibu na mchezaji huyo vinasema Pato yupo tayari kukubali ofa hiyo na muda sio mrefu wataweka wazi juu ya mkataba wake.

## UNITED YAKANUSHA KUWASILIANA NA RAMOS

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeripoti kuwa haijawasiliana na Sergio Ramos licha ya uwepo wa taarifa kwamba, mashetani wekundu hao wana nia ya kumleta beki huyo wa Real Madrid, pale Old Trafford.


Mkataba wa Ramos kule kwenye dimba la Bernabeu unamalizika Juni mwaka huu, na inaonekana kuna uwezekano mkubwa mchezaji huyo wa Hispania akaondoka pale Los Blancos kabla ya msimu mpya wa 2021-22.

United imekuwa ikihusishwa zaidi na mchezaji huyo mwenye miaka 34, ambaye anatarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi Aprili mwaka huu, kutokana na jeraha la goti ambalo linahitaji upasuaji.

Hata hivyo, kwa mujibu wa mwandishi wa habari wa Italia, Fabrizio Romano, mabingwa hao wa England mara 20, bado hawajawasiliana na Ramos, na inatajwa wanaendelea kufanya tathmini.

Nyota huyo wa zamani wa Sevilla amedaiwa tayari amekataa ofa mbili za mkataba mpya kutoka kwa upande wa kikosi hicho kinachonolewa na kocha, Zinedine Zidane na hivi karibuni ameendelea kuwa karibu zaidi na mlango wa kutokea hapo.

Ramos ambaye anaaminika kuwa analengwa na Paris Saint-Germain ya Ufaransa, ameifungia Los Blancos mabao 100 katika mechi 668 za mashindano yote, akishinda mataji matano ya Ligi Kuu Hispania, LaLiga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.



## HABARI MICHEZO



# UNITED
## WAFIKIRIA MKATABA WA SOLSKJAER

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United wameripotiwa watasubiri hadi majira ya joto kabla ya kufanya mazungumzo ya kumwongezea mkataba mpya kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer.

Nyota huyo wa zamani wa Norway hapo awali alikuwa chini ya shinikizo kubwa la kutetea kibarua chake pale Old Trafford hadi klabu ilipoibuka kuwa wapinzani wa taji la Ligi Kuu England mwishoni mwa mwaka.

United kwa sasa wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikiwa ni alama tano tu nyuma ya majirani zao Manchester City, ambao pia wana mchezo mmoja mkononi.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, Makamu Mwenyekiti Mtendaji wa United, Ed Woodward hatashinikiza mazungumzo juu ya makubaliano mapya ya mkataba wa kocha huyo hadi mwisho wa msimu.

Msimamo huo umekuja licha ya Solskjaer kuwa amebakiza chini ya miezi 17 kwenye mkataba wake, na kuiweka klabu mbioni kufikiria mchakato wa mkataba mpya.

Solskjaer amepata ushindi katika mechi 70 na kupoteza mechi 29 kwenye jumla ya michezo 125 aliyoiongoza United.

# Liverpool waambiwa wamsajili Kane

**LIVERPOOL, England**

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool, Stan Collymore amewataka mabingwa watetezi Ligi Kuu England, kumsajili Harry Kane kutoka Tottenham Hotspur katika dirisha lijalo la majira ya joto, kama wanataka kushindana na Manchester City kuwania tena ubingwa msimu ujao.

Ushindi wa mechi mbili katika michezo yao tisa ya mwisho ya ligi imewaacha vijana wa Jurgen Klopp wakiwa nyuma ya alama 10 dhidi ya vijana wa Pep Guardiola, ambao waliongeza ushindi wao kuwa mechi 14 wikendi iliyopita pale Anfield.

Akichangia kwenye safu ya gazeti la Daily Mirror, Collymore anasema Liverpool wanatakiwa kuendana na matumizi ya City katika dirisha la uhamisho ili waendelee kusalia na ushindani wa taji msimu ujao.

**"Wanahitaji kuamka na kuinusa kahawa, ambayo inamaanisha wamiliki kuhakikisha wanatumia fedha sawa na City katika kipindi hicho.**

"Inamaanisha kwamba kama City itaenda kumnunua Erling Braut Haaland msimu huu wa joto, basi Liverpool lazima imnunue, Robert Lewandowski au hata kuweka zabuni kumnasa Harry Kane."

Collymore amesisitiza kuwa kitu ambacho Liverpool hawapaswi kufanya ni kukaa na kusema kuwa wana kikosi kizuri chipukizi cha vijana, ambao wanaweza kuwatumia kuendana na changamoto, kwa kuwa timu nyingi zinawekeza kwenye soko hata kama zinakuwa na vijana.

# Mo Salah atajwa Bayern Munich

**MUNICH, Ujerumani**

MKURUGENZI Mkuu wa Bayern Munich, Karl-Heinz Rummenigge amebainisha kuwa itakuwa "heshima" kumsajili mshambuliaji wa Liverpool, Mohamed Salah, lakini amesema hawana mpango wowote wa kumleta Ujerumani.

Salah, ambaye alijiunga na Liverpool kutoka AS Roma ya Italia mwaka 2017, amekuwa bora zaidi chini ya Jurgen Klopp na kuwa mmoja wa washambuliaji bora duniani.



Nyota huyo wa kimataifa wa Misri amezivutia klabu nyingi kubwa Ulaya, huku Rummenigge akimtazama nyota huyu mwenye umri wa miaka 28 kwa kumlinganisha na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

"Kwa maoni yangu, Salah ndiye Messi wa Afrika na kwa kweli ana ujuzi wa kucheza kwa timu bora duniani," amesema Rummenigge akinukuliwa na ON Time Sports.

"Alichofanikiwa kinaweza kulinganishwa na kile ambacho Messi na Ronaldo wamekifanya kule Barcelona na Real Madrid.

"Kwa sasa hatuna mpango wa kumsajili Salah, lakini kwa kweli itakuwa heshima kuwa naye."

Nyota huyo kwa sasa ndiye mfungaji anayeongoza kwenye Ligi Kuu England, akicheka na nyavu mara 16 katika michezo 22 aliyocheza.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL AFUNGUKA KUMPA NAFASI KEPA

Ndiye golikipa chaguo la kwanza sasa katika kikosi cha Chelsea baada ya Mjerumani huyo...

**LONDON, England**

THOMAS Tuchel amemwambia, Kepa Arrizabalaga asiwe na presha kubwa kwa sababu sasa ana nafasi ya kuanza "maisha mapya" chini ya raia huyo wa Ujerumani.

Kepa alikuwa golikipa ghali zaidi wakati alipojiunga na Chelsea akitokea kwa miamba ya LaLiga, Athletic Bilbao kwa ada iliyoripotiwa kuwa ni pauni milioni 71.6, miaka miwili iliyopita.

Hata hivyo, nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 hakuwa kwenye kiwango cha kuvutia na nafasi yake ikachukuliwa na Edouard Mendy, ambaye alisajiliwa kutoka Rennes, Septemba mwaka jana.

Kepa ameanza mechi zote za Chelsea za Kombe la FA msimu huu na Tuchel amethibitisha kwamba ataendelea kupewa nafasi kubwa ya kucheza.

Tuchel, ambaye amecheza mechi tatu za Ligi Kuu England kati ya nne tangu achukue mikoba ya Frank Lampard mwezi uliopita, amempa changamoto Kepa kusahau kuhusu kipindi kigumu alichokipitia hapo England na kumtaka kuanza maisha mapya. "Tumeangalia hali yake na magumu aliyokuwa nayo kwenye mchezo," alisema Tuchel.

"Pengine, pia hali ya uhamisho wake kwa kiasi fulani ulikuwa mzito mabegani mwake. Jambo zuri kwake ni kwamba haya ni maisha mapya kwa upande wake kwa sababu sina historia nae.

"Ni nafasi maalumu. Kama unafanya makosa, kila mmoja anaona na kuzungumza kuhusu hilo, hivyo unahitaji nafasi ya kuonyesha ubora na uimara wako.

"Nimeona hilo kwa magolikipa wote watatu. Bila shaka naamini Kepa anaweza kubadilika na kuwa kwenye kiwango bora kabisa."

## KWA UFUPI

**POCHETTINO: HATUJAKOSEA**

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino amesisitiza klabu yake na wachezaji hawajaonyesha "utovu wa nidhamu" kwa kuzungumzia nia yao ya kumsajili mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi ***(ESPN)***

**CITY YASAKA STRAIKA**

MANCHESTER City itamsajili mshambuliaji mpya majira ya joto yajayo kama wakifanikiwa kumshawishi, Lionel Messi, huku straika wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, akiwa kipaumbele. ***(90 Min)***

**DORTMUND KUUZA SABA**

KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kuwauza wachezaji saba kipindi kijacho cha majira ya joto, akiwamo winga, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20. ***(Mirror)***

**WITSEL, JUDE SOKONI**

KIUNGO wa Ubelgiji, Axel Witsel mwenye umri wa miaka 32, straika wa Marekani, Giovanni Reyna ambaye ana umri 18 na kiungo wa England, Jude Bellingham (17), ni miongoni mwa wachezaji watakaouzwa na Borussia Dortmund ili kupata fedha. ***(Waz, via Express)***

**TUCHEL AMTAKA RUIZ-ATIL**

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel amemtaka kiungo wa kati wa PSG, Kays Ruiz-Atil mwenye umri wa miaka 18 kumfuata kule Stamford Bridge. ***(Foot Mercato, via Team Talk)***

**MOURINHO AMTETEA DELE**

KOCHA Jose Mourinho amekiri kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Dele Alli (24), yawezekana amevurugwa na uvumi unaomhusisha yeye kuondoka Tottenham Hotspur. ***(London Evening Standard)***

**RAPHINA ANUKIA LIVERPOOL**

KLABU ya Liverpool ina mpango wa kumsajili winga wa Leeds United, Raphinha ambaye ana umri wa miaka 24. ***(France Football, via Mail)***

**UDINESE: DE PAUL HAUZWI**

KLABU ya Udinese haijaamua kumuuza kiungo wake wa kati, Rodrigo de Paul mwenye umri wa miaka 26, baada ya taarifa zinazomhusisha mchezaji huyo kuhamia Liverpool wakati wa dirisha la usajili la Januari. ***(Goal)***

**BROM YAMTOSA MUSA**

KLABU ya West Brom imeamua kusitisha mpango wa kumpa mkataba, Ahmed Musa baada ya mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Nigeria mwenye umri wa miaka 28 kufanya majaribio na timu hiyo. ***(Express & Star)***

**TERRY NJIA MOJA**

KOCHA msaidizi wa Aston Villa, John Terry yuko kwenye orodha ya watakaochukua nafasi ya kocha mkuu wa Bournemouth. ***(Birmingham Mail)***

**VIEIRA KUREJEA EPL**

KOCHA wa zamani wa Nice na kiungo wa kati wa zamani wa Arsenal, Patrick Vieira ni miongoni mwa wanaowania nafasi ya kocha wa Bournemouth. ***(TalkSport)***

HABARI MICHEZO

# NAMUNGO YAENDA ANGOLA IKIACHA 'MAJEMBE' MANNE

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika, Namungo FC wanatarajia kuondoka nchini leo kuelekea Angola kuwafuata wenyeji wao CD Primeiro De Agosto bila nyota wake wanne wa kikosi cha kwanza, imefahamika.

CD Primeiro De Agosto itaikaribisha Namungo katika mechi ya kwanza ya hatua ya mtoano itakayochezwa keshokutwa nchini humo.

Nyota hao ambao wameachwa katika msafara wa timu hiyo ni pamoja na Blaise Bigirimana, Abdulhalim Humud, Amani Kiata na Adam Salamba.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Katibu Mkuu wa Namungo FC, Ally Suleiman, alisema kikosi cha timu hiyo kimeondoka na wachezaji 23 na baadhi ya nyota walioachwa inatokana na kuwa majeruhi pamoja na matatizo ya kifamilia.

Suleiman alisema Humud na Amani Kiata wamelazimika kubaki kwa sababu ya matatizo ya kifamilia wakati Bigirimana ni majeruhi huku Salamba akiwa kwenye mchakato wa kuondoka kuelekea Serbia ambako ameuzwa.

"Salamba amepata timu nchini Serbia na sasa kuna mambo tunaweka sawa kwa ajili ya kukamilisha ofa yake ya kwenda nchini huko, baada ya kukamilika tutaweka wazi hiyo timu kwa sababu muda wowote kuanzia wiki hii anatakiwa kuondoka," alisema Suleiman.

Aliongeza kikosi cha timu hiyo kiko vizuri na wamejiandaa kwenda kupambana kutafuta matokeo chanya mbele ya wapinzani wao, De Agosto.

"Kocha ameona mapungufu ya kikosi chake na kufanyia kazi, lakini ameona ubora na madhaifu ya wapinzani wetu kupitia CD na mitandaoni katika baadhi ya mechi walizocheza," alisema katibu huyo.



Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Haji Manara (kushoto), akifanya mahojiano na waandishi wa Kituo cha Televisheni cha Taifa cha Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kuelekea mchezo wa Kundi A wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita utakaochezwa leo usiku jijini Kinshasa. **PICHA: MTANDAO**

# Rage ashangazwa 'nyundo' za TFF

**Na Adam Fungamwangwo**

BAADA ya Kamati ya Maadili ya Shirikisho la Soka Nchini (TFF), kutangaza kuwafungia viongozi watatu wa vyama vya soka vya mikoa, aliyekuwa Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Ismail Aden Rage ameshangazwa na 'fungia' hiyo na kusema haina afya kwa soka la Tanzania.

Juzi kamati hiyo ilitangaza kumfungia Mwenyekiti wa Chama cha Soka Shinyanga (SHIREFA), Bannister Rogora, Mgombea Uenyekiti wa Chama cha Soka Mkoa wa Tabora (TAREFA), Dickson Mulimuka na Stella Maganga ambaye alikuwa anawania uongozi SHIREFA kwa sababu mbalimbali za kimaadili.

Rage alisema hapingi adhabu kwa sababu zipo kikanuni, lakini anachoshangazwa ni kuwafungia tena kwa miaka mingi, kitu ambacho hakimsaidii yeyote yule kati ya pande hizo.

"Adhabu ya miaka 10 ni mingi mno, unapata faida gani? Haiisaidii kamati, TFF, wala aliyefungiwa. Hebu angalia hata adhabu za FIFA, wanatoza faini tu. Mimi nadhani kamati zingekuwa zinatoza faini ili kutunisha mfuko wa maendeleo ya soka badala ya kufungiana," alisema Rage.

Mwenyekiti huyo wa zamani wa Simba alisema kwa jinsi ilivyo sasa, TFF haiwezi kuingilia chochote kile kwa sababu kamati ziko huru, ila waliofungiwa wanaweza kukata rufani.

Kamati hiyo ilimfungia Rugora kwa miaka miwili kwa kosa la kumteua mwakilishi wa klabu, Michael Kaijage kuwa Kaimu Katibu Mkuu badala ya Katibu Msaidizi, Stephen Mihambo.

Mulimuka yeye amefungiwa kutojishughulisha na soka kwa miaka 10 kwa sababu ya kusimamia uchaguzi wa Chama cha Soka Wilaya ya Urambo jambo ambalo ni kinyume cha mwongozo wakati Stella amefungiwa kwa muda wa miaka 10 kwa kosa la kuwa mgombea, msimamizi na mpigakura katika uchaguzi wa TAREFA.

## Mzunguko wa pili Z'bar Februari 20

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MZUNGUKO wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar umepangwa kufanyika kuanzia Februari 20, mwaka huu, visiwani humo.

Hata hivyo, msimu huu ligi hiyo itaendelea bila ya kufunguliwa kwa dirisha dogo la usajili kutokana na Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba kukwama.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar (ZBL), Sheha Mohamed, alisema sasa dirisha dogo litafunguliwa baada ya Ligi Daraja la Kwanza ya Pemba itakapoanza kuchezwa.

Mohamed alisema kuanza kwa mzunguko huo bila ya kufunguliwa kwa dirisha dogo ni uamuzi uliopewa baraka na timu zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar baada ya kufanya kikao cha pamoja na ZBL.

"Hatuwezi tukafanya usajili wa dirisha dogo hali ya kuwa Pemba wamegoma kucheza ligi, na kifupi tangu msimu ulipoanza Kanda ya Pemba haikuchezwa, hivyo timu haiwezi kuingia katika dirisha dogo," alisema Mohamed.

Timu zinazoshiriki Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba zimeingia katika mgomo wa kutocheza wakiwa na madai mbalimbali ikiwamo kutomtaka Rais wa Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), Seif Kombo Pandu.

## Taifa Jang'ombe yaongoza Unguja

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Dulla Boys katika mechi ya Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, timu ya Taifa Jang'ombe imefanikiwa kukaa kileleni katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 19 mkononi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Taifa Jang'ombe, Mustafa Hassan 'Kocha Muu' alisema matarajio yake ni kuona anamaliza mzunguko huu wa kwanza bila ya kutopoteza mchezo hata mmoja.

Kocha huyo alisema kwa sasa anakiimarisha kikosi chake ili kuhakikisha kinaendelea kuvuna pointi tatu kwenye kila mechi watakayocheza na kujiweka sehemu salama.

Alisema Ligi Daraja la Kwanza ni ngumu na hali hiyo inatokana na timu zote kufanya usajili wa wachezaji bora wenye uzoefu na vijana ambao bado wana nguvu ya kucheza mpira wa ushindani.

"Tunapambana ili kuona tunatoka na ushindi katika mechi zetu zote, tunajua ligi hii ni ngumu tofauti na mashabiki wanavyoiangalia, ligi yetu ina ushindani wa hali ya juu na wachezaji wanajituma vyema katika timu zao," alisema kocha huyo.

Hata hivyo alisema ni mapema kusema kama timu hiyo itapanda daraja na kuelekea Ligi Kuu msimu ujao ingawa malengo yake ni kuona wanakata tiketi ya kushiriki Ligi Kuu Zanzibar.

Michezo

Ijumaa Februari 12, 2021

Nipashe



TUCHEL AFUNGUKA KUMPA NAFASI KEPA

HABARI UK 22

# SIMBA, AS VITA MECHI YA KISASI

●●●Mnyama atamba hasumbuliwi na rekodi, ajipanga kucheza kwa tahadhari...

**Na Saada Akida**

HATIMAYE ile siku iliyokuwa inasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka nchini imefika kwa wawakilishi wa Tanzania, Simba kuwakabili wenyeji AS Vita katika mechi ya kwanza ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Stade des Martyrs uliokо Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Mara ya mwisho timu hizo zilipokutana katika mashindano hayo Simba iliibuka na ushindi wa mabao 2-1 na kutinga hatua ya robo fainali huku ikiwatoa kwenye michuano hiyo, Wakongomani hao ambao katika mchezo wa kwanza waliwapa kichapo cha mabao 5-0.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes alisema kikosi chake kimejiandaa kucheza kwa tahadhari ili kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu katika mchezo huo ili kufikia malengo waliyonayo.

Gomes alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wake wako tayari kwa ajili ya kupambana na kutafuta matokeo chanya, lakini wakiheshimu wapinzani wao ambao wanarekodi nzuri wanapokuwa kwenye uwanja wa nyumbani.

"Nawafahamu AS Vita, najua uwezo na kocha wao Jean Florent Ibenge, hivyo hatutacheza kwa kufunguka sana, tutashambulia pamoja na kukaba kwa kutowapa nafasi wapinzani wetu kutushambulia zaidi, najua itakuwa ni mechi yenye ushindani."

"Wenzetu wanacheza nyumbani hivyo wanafaida hilo halitaturudisha nyuma na tayari wachezaji wako fiti kutafuta matokeo katika mechi ya kesho (leo)," alisema Gomes.

Naye Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugezi Simba, Salim Abdallah 'Try Again', alisema malengo ya awali ya timu yao yalikuwa kucheza hatua ya makundi na sasa akili na nguvu zao wameziimarisha kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo huo na kutorudia makosa ya misimu miwili iliyopita.



Magolikipa wa Simba, Aishi Manula (mwenye mpira) na Beno Kakolanya (kulia), wakiwa katika mazoezi ya kujiandaa na mechi ya Kundi A ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), itakayochezwa jijini Kinshasa leo usiku. **PICHA: MTANDAO**

Salim alisema ana imani kubwa na timu hiyo itafanya vizuri katika michuano hiyo na kusonga mbele kulingana na maandalizi ambayo benchi la ufundi linaloongozwa na Gomes wamefanya.

"Mipango yetu msimu huu ni kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara, kufika hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika ambayo tayari tupo, sasa tunapambana kuhakikisha tunapata pointi ambazo zitatupeleka kucheza nusu fainali, kikubwa ni kusimamia nidhamu ya wachezaji, hatuwezi kufikia malengo hayo tusipokuwa na nidhamu," alisema kiongozi huyo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, aliliambia gazeti hili wanaiheshimu AS Vita na wanafahamu ni ngumu kucheza nao wakiwa nyumbani lakini wao wamefuata matokeo chanya.

"Hatukuja huku kumwogopa mtu, heshima yetu ni ya kimchezo na hatuiangalii historia ya mechi iliyopita ya hapa Kinshasa. Kocha wetu ni mwerevu na atakuja na 'plan' sahihi ya kucheza mechi ya ugenini kama hii," alisema Manara.

Aliongeza kambi ya wachezaji hiyo ina utulivu na kila mmoja akili yake ni kujitoa kupata ushindi katika mechi hiyo ya kwanza ambayo itawapa picha ya kukamilisha 'hesabu' za kusonga mbele.

Naye nahodha wa AS Vita, Jereme Mumbele aliliambia gazeti hili wamejipanga kuanza vyema hatua hiyo ya makundi kwa sababu wanataka kumaliza katika nafasi mbili za juu kwenye kundi hilo.

Mumbele alisema timu zote walizopangiwa nazo ni nzuri, hivyo wanatarajia kukutana na mechi zenye ushindani.

"Tumejipanga kuchukua pointi zote za nyumbani, pointi tisa za nyumbani na sare za ugenini ndio zitatuvusha, tumejipanga kwa hilo," Mumbele alisema.

Mechi nyingine ya kundi hilo itachezwa Februari 16, mwaka huu, kati ya vigogo wa Misri, Al Ahly dhidi ya El Merreikh ya Sudan huku Simba ikirejea nyumbani itaendelea na michezo yake ya Ligi Kuu Tanzania Bara na baadaye itawakaribisha Al Ahly kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ifikapo Februari 23, mwaka huu.

## YANGA YATAMBA, AZAM YACHAPWA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga wakitamba wataendelea kutoa 'dozi', Azam FC imeendelea kujiweka katika nafasi ngumu kwenye mbio za kuwania ubingwa wa ligi hiyo baada ya kufungwa mabao 2-1 na Coastal Union katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga jana.

Yanga itakuwa ugenini kesho dhidi ya Mbeya City katika mechi ya raundi ya 19 ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Ofisa Uhamasishaji wa Yanga, Antonio Nugaz alisema kikosi chao kiko imara na kimekwenda Mbeya kwa kazi moja ya kuhakikisha wanapata pointi tatu.

"Tumejipanga kuendelea pale tulipoishia, kikosi kimeshatua salama jijini Mbeya kwa ajili ya mchezo wetu wa Jumamosi, tunawaomba mashabiki wetu wajitokeze kwa wingi ili kuwaongezea morali wachezaji wetu, tunaahidi tutaendelea kuwapa furaha, msimu huu tuna jambo letu," alisema Nugaz.

Katika mechi ya kesho, Yanga itamkosa kiungo mshambuliaji wake, Saidi Ntibazonkiza aliyebakia jijini Dar es Salaam kutokana na kutokuwa 'fiti' lakini akiendelea na programu maalumu ya mazoezi ya 'gym'.

Bao la Hamad Majimengi lililofungwa dakika ya 54 ndio liliipatia Coastal Union ushindi dhidi ya Azam FC na kuwafanya mabingwa hao wa Tanzania Bara mwaka 1988 kufikisha pointi 23.

Wenyeji Coastal Union ndio walikuwa wa kwanza kupata bao dakika ya tisa kupitia kwa Haji Ugando aliyefunga kwa penalti na Daniel Amoah kuisawazishia Azam dakika 36 na kufanya timu hizo kwenda mapumziko wakiwa sare ya bao 1-1.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa mapema jana mchana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Kagera Sugar ililazimishwa sare ya bao 1-1 na Gwambina FC kutoka Mwanza.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002